

USHAWISHI



Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu;
Amini tu, amini tu,
Mambo yote yawezekana, amini tu.

² Hebu tuinamishe vichwa vyetu. Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru Wewe kwa ajili ya wimbo huu, kuamini tu! Mwone tu Bwana wetu jinsi Yeye alivyomjia yule mvulana aliyekuwa na kifafa, kasema, “Ninaweza, kama ukiamini, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwao waaminio.” Bwana, saidia kutokuamini kwetu usiku wa leo, ndilo ombi letu. Tuna shukrani tele Kwako kwa ajili ya Uwepo Wako pamoja nasi, na kwa ajili ya watu wanaokuamini Wewe na kukupenda Wewe. Na kujua sasa, si tutakuwa, bali sasa tumeinuliwa juu katika mahali pa Mbingu ndani ya Kristo Yesu, tukiketi karibu na Mfalme wetu usiku wa leo, tayari tumeketi mahali petu pamoja na Yeye. Loo, jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya imani hii tulioyo nayo katika Yeye, ahadi Zake, tukijua kwamba kamwe haziwezi kushindwa, kwamba daima ni kweli. Tunaomba ya kwamba Wewe utatutembelea usiku wa leo. Jalia Roho Mtakatifu alichukue Neno la Mungu na kuligawa Hilo kwa mioyo yetu kama tu tulivyo na haja, hata wakati tutakapoondoka usiku wa leo, tukienda kwenye makazi yetu, tuweze kusema pamoja na wale waliotoka Emau usiku mmoja, kasema, “Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo Yeye alipozungumza nasi njiani?” Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

³ Mwaweza kuketi. Nina furaha sana kurudi tena usiku wa leo, kuwazungumzia nyinyi na kushiriki pamoja nanyi, katika mambo ambayo ni ya Kristo. Hakuna kusudi jingine tulilo nalo la kuwa hapa, ila kufanya hilo, kushirikiana tu kwenye Neno Lake.

⁴ Ninasikitika mimi huwaweka nyote muda mrefu sana kila usiku. Mtu fulani aliniambia, kasema, “Watu huenda nyumbani hapa kwenye saa mbili u nusu au saa tatu, kutoka kanisani.” Bali mimi—mimi ni mkusini tu, na kidogo ni mwenda pole, mwajua. Na siwezi kuliwazia upesi sana. Inanibidi tu kwa njia fulani kuchukua muda wangu nalo.

⁵ Bali kwa hakika nina shukrani kwa ajili ya ushirikiano mzuri ambao . . . ambao ninapata kutoka kwenu enyi watu humo ndani, ambao wanamwamini Mungu. U—ushirikiano wenu mzuri hulifanya rahisi sana, pia, kwa Roho Mtakatifu kutembea miongoni mwa watu. Laiti ningaliweza kupata huu kila mahali, na—natamani, ambapo ungeweza kupata watu wanaoamini.

Haijalishi kile Mungu afanyacho, kiasi gani cha karama Yeye angeweza kuwakilisha, inakubidi kuiamini, unaona, kwa sababu haina nguvu isipokuwa uiamini.

⁶ Yesu wakati mmoja, akija kutoka nchi nyingine, aliingia katika nchi Yake Mwenyewe. Na wao wakasema, “Tulisikia Wewe ulifanya *hiki na hiki* mahali fulani,” lakini basi Yeye asingeweza kufanya kazi nyingi kuu. Sasa hatupendi kusema hilo namna hiyo, lakini hivyo ndivyo Maandiko yanavyolisema, kwamba Yeye angefanya... “Yeye asingeweza kufanya kazi nyingi kuu, kwa sababu ya kutokuamini kwao.”

⁷ Na nguvu za Mungu kikomo chake ni imani yako katika Hizo. Unaona? Hicho ndicho kipimo tu zilizo nazo, ni imani yako. Na ikiwa... Mambo yote yanawezekana kwao ambao wataliamini. Unaona? Yupu Mungu mkuu Mbinguni, na iwapo tungeweza tu kuingia katika mawasiliano, kama mkondo wa moja kwa moja Kwake, mambo yote yanawezekana. Unaona? Bali lazima tuingie katika mahusiano na Yeye, bila ya kukwama mahali popote, mkondo tu ulio wazi kati yetu na Mungu. Ndipo Yeye akasema, “Ukiuambia mlima huu, ‘ng’oka,’ na usitie shaka moyoni mwako, bali uamini kwamba kile ambacho umesema.” Sasa, huwezi kumpumbaza. Shetani hapumbaziki kwa urahisi sana, kwa hivyo huwezi kumpumbaza. Lakini wakati kweli unalijua, basi halina budi kutendeka, unaona, lazima tu litendeka.

⁸ Kwa hiyo tupo hapa, na kumwabudu Yeye, na Yeye ni wa kupendeza na mzuri kuliko kumi ya maelfu kwa nafsi yetu. Na hakika tuna furaha kuketi hapa pamoja nanyi, usiku wa leo, katika wakati huu mzuri wa ushirika.

⁹ Sasa, nyinyi mnaopenda kusoma Neno, ama kutia alama sehemu hizo. Nilifikiria usiku wa leo, nimekuwa nikihubiri sana juu ya uponyaji wa Kiungu, kwa namna fulani nimebadilisha somo usiku wa leo, kidogo. Si hasa kulibadilisha, ila tu mwendelezo wake. Kwa sababu, huwezi kubadilisha Neno moja katika Biblia, kwa sababu linaingiana tu na Maneno mengine pamoja na Hilo. Maandiko yote hushikamana tu pamoja. Ni kama tu ninii—ninii... .

¹⁰ Samahani, kama hili linasikika la kukufuru, na mimi nisingelimaanisha hivyo, hata kidogo. Lakini ni kama tu mchezo-fumbo, mwajua. Tulizoea ku—kuikatakata maskini michezo-fumbo, na halafu tungeketi chini na kuchunguza jinsi ya kuuweka pamoja. Na ndipo ingetubidi kuwa na kitu fulani kimewekwa kando, picha ya kile tulichokuwa tunajaribu kuweka pamoja, kufanya mchezo-fumbo utokee vizuri. Kama hukufanya hivyo, unge—usingefaulu kamwe kufanya hivyo.

¹¹ Na sasa hivyo ndivyo Maandiko yalivyo. Yamekatwakatwa namna hiyo, kufichwa kutoka kwa macho ya wenye hekima na akili; unaona, wao ni kama Mafarisayo, wasomi wenye akili. Na

Yesu alimshukuru Mungu kwamba (Hilo) Yeye alikuwa ameficha Hilo kutoka kwa macho yao, na atalifunua Hilo kwa watoto watakaojifunza.

¹² Sasa kama unataka mfano wako, kuweka kando mchoro wako, kuona kile Maandiko yanayoendana nacho, mweke tu Yesu hapa na uanze kumwambia Yeye, na kuuweka katika Biblia. Utapata kitu chote kikitokea vizuri, maana ni ufunuo wa Yesu Kristo. Ninii—Agano Jipya na la Kale, yote mawili, yote hunena juu ya Yesu, unaona, Yesu Kristo Mwana wa Mungu, maana Yeye ni (ndiye) Kitabu hiki cha Ukombozi. Yeye alikuwa ni Neno, na Yeye ni Neno, na hilo halina budi kuwa ni Yeye, unaona. Kwa hiyo hiki ndicho Kitabu chote cha Ukombozi, ambacho ni Yesu Kristo, aliyewekwa pamoja vizuri na Mungu; pamoja na ahadi za ukombozi na uponyaji, na kila kitu, kwa ajili ya mwanadamu. Unaona? Je! mnapata hilo sasa? Kitabu hiki ni Yesu Kristo, aliyewekwa pamoja na Mungu. Unaona? Na Yeye alikuja kama mwanadamu na kutukomboza, na kila ahadi imo ndani Yake, na kwa ajili yako, kwa kuwa Yeye ndiye Mkombozi.

¹³ Hebu tugeukie usiku wa leo kwenye Agano la Kale, kupata kile ambacho tungependa kutolea fungu letu, tunaposoma kutoka katika Isaya, mlango wa 6 wa Kitabu cha nabii Isaya.

¹⁴ Ninapenda maandiko ya Isaya. Alikuwa nabii mashuhuri. Je! mliwahi kujua kwamba Isaya aliandika Biblia yote, katika kitu kama utangulizi Wake? Aliandika. Isaya anaanza katika uumbaji, katikati ya Kitabu akaja Yohana Mbatizaji, na mwisho katika Utawala wa miaka Elfu. Kwa hiyo yeye. . . Kuna Vitabu sitini na sita vya Biblia, na milango sitini na sita ya Isaya, kwa hiyo kwa hakika ni kielelezo tu cha Biblia yote.

¹⁵ Sasa hebu tusome kutoka kwenye mlango wa 6.

Katika mwaka ule...aliokufa Uzia nalimwona Bwana ameketi katika kiti cha enzi, juu...kuinuliwa sana, na pindo za vazi lake zikalijaza hekalu.

Na juu yake walisimama maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.

Wakaitana kila mmoja na mwenzake, wakisema, Mtakatifu, mtakatifu, ni BWANA Mungu wa majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.

Na misingi ya vizingiti ikatikisika kwa sababu ya sauti yake, aliyelia, nayo nyumba ikajaa moshi.

Ndipo niliposema, Ole wangu! Kwa maana nimepotea; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu, nami ninakaa kati ya watu wenye midomo michafu; na macho yangu yamemwona Mfalme, BWANA wa majeshi.

Kisha mmoja wa maserafi wale akaruka akanikaribia, naye alikuwa na kaa la moto mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitwaa kwa makoleo toka juu ya madhabahu;

akanigusa kinywa changu kwa kaa hilo, akaniambia, Tazama, hili limekugusa midomo yako, na uovu wako umeondolewa, na dhambi zako zimesafishwa.

Tena nikasikia sauti ya Mungu...sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakaye... ama ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.

16 Ningependa kuchukua fungu, kama tungeliita hivyo, juu ya somo la *Ushawishi*. Ushawishi ni kitu kikubwa. Tunaambiwa kuhusu, Andiko, kwamba, “Sisi ni nyaraka zilizoandikwa, na kusomwa na watu wote.”

17 Basi sisi, kama Wakristo, daima tunapaswa kuchunguza kile tunachofanya na kile tunachosema, kwamba sisi ni waaminifu kabisa kwa kila mtu. Na wewe, ikiwa huwezi kuwa mwaminifu na mwanadamu mwenzako, kwa hakika hutakuwa mwaminifu na Mungu. Kwa hiyo jinsi tunavyomtumikia Mungu, ni, tunatumikiana mmoja na mwenzake. Mwaminifu kama vile ningeweza kuwa na wewe, hivyo ndivyo nitakavyokuwa mwaminifu na Mungu. Na vivyo hivyo na wewe kwangu mimi. Lazima tuwe waaminifu na kila mmoja katika shughuli zetu zote.

18 Na mtu fulani anatutazama. Huenda usifikirie hivyo, lakini kuna macho yanayokutazama. Na maisha yako yanamshawishi mtu fulani. Labda ni mtoto mchanga, na mtoto huyo huenda akakua kuwa Finney mwingine, au Moody, ama kadhalika. Hatujui. Lakini ma—maisha yako yanamshawishi mtu fulani.

19 Basi mandhari yetu usiku wa leo ni mandhari ya kipekee sana juu ya hili, kwa sababu kulisoma tu alasiri ya leo, wakati nilipokuwa nikisoma, nilikuwa nikiwazia jinsi Mungu alivyo mkuu.

20 Asubuhi ya leo, wakati mimi na mwanangu kwa namna fulani tulikuwa tunatembea kuzunguka je—jengo, kulikuwa na watu wengi sana. Tuliteremka chini kuzunguka Times Square, kwa kuwa walisema walikuwa wanaenda kuliporomosha. Nafikiri u...ka—kazi tayari imeanza. Kwa hiyo nilikuwa nikitazama hiyo, na tulikuwa tukipiga picha. Na watu, wakisongamana! Nilimwambia mwanangu, Billy, nikasema, “Wote wanaenda wapi? Haraka ya nini? Hawa hapa, chini yetu, wanakimbia; na hapa, wanakimbia; na juu yetu, wanakimbia. Mimi... Kila mtu anaenda wapi kwa haraka hivi?”

21 Na tuliposimama, tuliwazia hili, “Mungu anawezaje kujua mawazo ya kila mtu? Na ingewezekanaje kuwa kwamba ma—

mabilioni yote duniani, na hata hivyo Mungu anajua kila wakati unapopepesa jicho lako?” Yeye hana kikomo.

²² Na ikiwa unataka tu kujua, na kuridhisha tu hilo, kama likiwahi kuja niani mwako, nenda nje na utazame juu kwenye nyota na kushangaa jinsi Yeye hudhibiti hizo zote, ndipo unaona jinsi hii ingekuwa kazi ndogo. Wakati hizo nyota, unaweza kuona kipindi cha miaka milioni mia moja na ishirini ya nuru, kupitia kioo; unajua jinsi nuru husafiri upesi, mbona, ungeweza kuendesha safu ya tisa-tisa kuzunguka jimbo la New York, usingeweza kuieleza katika maili. Na zaidi ya hapo ni nyota nyingi tu kama zilizvyo upande huu, huko kwenye Mlima Palomar na Mlima Wilson huko California, inaweza kuonekana.

²³ Wazia jinsi Yeye alivyo mkuu, na jinsi Yeye anavyoshikilia dunia! Dunia hii, ama moja ya nyota hizo ikiondoka mahali pake, umbali wa mamilioni na mabilioni ya maili, ingeathiri dunia hii. Mfumo huo wote wa jua hauna budi kukaa tu mahali pake. Basi, unaona, kila kitu ambacho Mungu aliumba, namna hiyo, humtii Mungu. Lakini wakati Mungu alipomwumba mwanadamu, mwanadamu anaonekana kutaka kujua zaidi kuliko Yeye anavyojua, unaona; ni, sisi ndio wa pekee nje ya mahali petu. Hivyo hukaa mahali pao. Na inabidi vikae mahali pao, kupatana na kila kimoja.

²⁴ Kwa mfano, mwezi, kama mwezi ungewahi kuondoka mahali pake, dunia ingejaa maji, katika dakika chache. Unaona, mwe—mwezi hasa ni—ni kama mwangalizi wa bahari. “Yeye aliweka mipaka yake, hata haiwezi kupita.” Basi wakati mwezi unapogeuka kutoka duniani, haya hapa yanakuja mawimbi. Kama mwezi haukuyashika upande ule mwingine, yangeijaza dunia. Unaona? Kwa hiyo mwezi hukomesha na—naye hugeuza mgongo wake kuangalia upande ule mwingine wa ulimwengu, ndipo—ndipo hapa yanakuja maji yakiingia upesi kwelikweli, na ndipo anageuka tena. Yeye ni mtumishi wa Yehova. Bahari inasimama na kurudi mahali pake tena, kwa sababu inaona msogeo mkamilifu wa Yehova.

²⁵ Loo, kama sisi tulio kanisani, kama washiriki wa Mwili wa Kristo, tungeweza tu kufanya kazi katika umoja namna hiyo, mngeona Kanisa kubwa na lenye nguvu la Mungu aishiye, wote katika utaratibu mmoja, wamejazwa na Roho Mtakatifu. Hilo si lingekuwa la ajabu? Kila mshiriki wa Mwili akifanya kazi sawa kabisa mahali pake, kila karama mahali pake, kila karama ikisaidia nyingine, kila mshiriki akimsaidia mwenzake, hilo lingekuwa ajabu. Hilo ndilo tunalotaka kuona. Bali tutalionasiku moja, na kama ni sahihi.

²⁶ Sasa, jamaa huyu kijana, Uzia, alikuwa ni mfalme. Lakini kabla hajawa mfalme... Alikuwa mfalme kwenye wakati wa Isaya, nabii. Na yeye alikuwa mvulana mchungaji; alipenda mwitu. Alikuwa ushawishi mkubwa juu ya—juu ya maisha

ya Isaya. Isaya alikuwa ni kijana, pia, nabii kijana tu. Na unasoma hadithi hiyo, ukitaka kuchukua Mambo ya Nyakati ya Pili 26, itakuambia. Jinsi ambavyo kwenye umri wa miaka kumi na sita, baada ya kifo cha baba yake mwenye haki, alikuwa... walimchukua na kumfanya mfalme juu ya Israeli. Kwenye umri wa miaka kumi na sita alianza kutawala. Na yeye alikuwa ameona ushawishi wa wazazi wake; mama yake alikuwa ni mwanamke mtauwa, na baba yake alikuwa ni mwanaume mtauwa, mbele yake. Basi, katika hilo, liliweka ushawishi ndani ya mtoto huyo kufanya kile kilichokuwa sahihi.

²⁷ Nawaambieni. Nafikiri, leo hii, tuna wimbi kubwa la jinai la watoto kote nchini, lakini, kwa kweli, nafikiri lilianza nyumbani. Na—nafikiri wazazi walianza kuachilia. Na ikiwa mtoto alikuwa amelelewa katika nyumba nzuri, ya kitauwa, ya mtindo wa kale; sisemi lingekwisha kabisa, hakika sivyo, bali kwa hakika ingempa mtoto huyo aina sahihi ya ushawishi. Nafikiri, mara nyingi, kwamba, nyumba ambazo watoto wamelelewa vibaya, wakakimbilia mtaani, na kujiishia tu wenyewe huku mama anakaa kwenye baa, au ninii... naye baba, na kadhalika. Hawamshughulikii mtoto huyu. Jambo jingine, hawampendi na kumpa mahaba, kumkuza. Ni mchanga. Inakubidi kumfundisha kupenda na kuheshimu, na kusoma Biblia.

²⁸ Ninawazia kuhusu Susanna Wesley. Nafikiri alikuwa na watoto kumi na saba. Nafikiri hiyo ni kweli. Lakini alipata saa mbili au zaidi, kila siku, kuomba. Chini kwenye mwi—mwisho wa gauni lake, ambapo wavulana wadogo walipiga magoti kumzunguka, kutoka hapo kulitoa John na Charles ambao walibadilisha mkondo wa ulimwengu, wakaokoa ulimwengu katika siku hiyo. Na yeye hakuwa na mashine ya kufulia nguo na mashine ya kukausha, kama tulivyo nazo leo hii, na mashine ya kuosha sahani, na kadhalika, ama mtumishi wa kike. Kitu ambacho... Alizifanya zote mwenyewe, lakini bado angepata muda kwa sababu alikuwa anaweka ushawishi kwa watoto fulani ambao hatimaye walibadilisha mkondo wa ulimwengu. Nafikiri huyo ndiye mama wa mtindo wa kale, nyumba ya mtindo wa kale, ambapo maombi na ufahamu wa Biblia.

²⁹ Ninaamini, Abraham Lincoln hakumiliki kitabu maishani mwake, mpaka alipokuwa mkubwa kutosha, ila Biblia na... Nafikiri ama kilikuwa ni Kitabu cha Foxe Cha Wafia Imani... Huenda nisiwe, huenda kilikuwa ni kitabu kingine. Nafikiri kilikuwa ni Safari ya Msafiri, kuwa sahihi. Kilikuwa ni Safari ya Msafiri, na—na Biblia. Unaona namna ya tabia hicho kiliumba?

³⁰ Acha tu niingie katika nyumba yako na kuona aina ya picha ulizo nazo ukutani mwako. Hebu niende katika nyumba yako au ofisi yako, na hebu tuone aina ya muziki unaocheza. Unaona? Kile unachosoma, kile unachotazama, kwa kweli ninaweza kukuambia kilichoko ndani yako, unaona,

kwa sababu hula kwenye hicho. Unaona? Na, loo, kwenye nyumba, kama tulifanya nyumba kuwa ya kupendeza zaidi, watoto wasingalitaka kutoroka. Yafanye mambo zaidi kwa ajili yao, ambapo wanajisikia kukaribishwa na pazuri na starehe nyumbani; ambapo, nyumbani, ni vigumu kwao kungojea mpaka watakapofika huko. Na hivyo ndivyo nyumba inavyopaswa kuwa.

³¹ Na mimi ninafikiri hiyo ndiyo aina ya nyumba ambayo hapana shaka Uzia alimolelewa, kwa sababu ya ushawishi wa wazazi wake watauwa. Na punde tu alipokuwa mfalme, alipuuza maoni yote maarufu na tofauti zote za kisiasa, na akaweka nia yake kwa ajili ya kitu kimoja: yeye angemtumikia Mungu, haidhuru! Tunahitaji wanasiasa wengine zaidi namna hiyo. Yeye, yeye alidhamiria kwamba alikuwa anaenda kumtumikia Mungu, kwa sababu hivyo ndivyo alivyolelewa, naye baba yake alimpa ushawishi ufaao, kwamba a—angeweza kumtumikia Mungu na kuishi.

³² Na ufalme wake ulikuwa mashuhuri sana mpaka, ninaamini, ulikuwa wa pili baada ya ufalme wa Sulemani. Ninaamini imetambulishwa kuwa wa pili baada ya ufalme wa Sulemani. Jinsi Mungu alivyombariki!

³³ Na huu ulikuwa ushawishi mkubwa juu ya nabii huyu kijana, Isaya, ambaye alikuwa hekaluni wakati huo, ama nchini. Na jinsi alivyoonekana, na jinsi Mungu angembariki mtu aliyechukua msimamo sahihi, akafanya jambo sahihi, alikuwa na nia sahihi na lengo sahihi, na alifanya jambo sahihi.

³⁴ Wakati mwingine unaweza kuwazia kwamba hailipi. Lakini kwa kweli inalipa. Haina budi kulipa. Huwezi kuwa unaenda mashariki na magharibi kwa wakati mmoja. Huwezi kuwa unaenda kulia na kushoto kwa wakati mmoja. Huenda ukafikiria unaenda njia nyingine, bali sivyo. Kwa hiyo kama utaweka nia—nia yako na macho, na madhumuni na malengo, maishani, juu ya jambo sahihi, huna budi kutokea juu ya jambo sahihi. Huwezi kushindwa. Unaona? Hiyo ndiyo njia ya pekee. Haijalishi ni kiasi gani unajaribiwa kufanya upande ule mwingine, geuza kichwa chako kutoka kwa hilo na ufanye jambo lililo sahihi. Na wewe—wewe unajua uko sahihi; unajisikia vema zaidi, na uko vizuri zaidi. Na hayo ndiyo yote katika hilo, inakubidi. . . unaenda kutokea sahihi. Ukianza kuenda magharibi, huendi—hutakuwa unaenda kaskazini, utakuwa unaenda. . . utakuwa unaenda magharibi. Na hivyo ndivyo ilivyo katika sahihi na lisilo sahihi.

³⁵ Basi Isaya aliona hili, na akaona kwamba Mungu alimbariki. Na jinsi yeye. . . mataifa yote, yaliyomzunguka, sifa yake ilienea kote kuingia Misri. Na jinsi mataifa hayakutaka vita na yeye, wao—wao waliona kwamba Mungu alikuwa pamoja na yeye. Kwa hiyo yeye alininii tu. . . Walimpelekea sadaka za amani na

kundi la kondoo, na vitu, na—na kumpa yeye, kuleta amani. Na yeye alikuwa ni mtu mwema.

³⁶ Na mimi ninaamini ikiwa taifa, au watu, au kanisa, ama mtu binafsi, haijalishi ni kiasi gani wakosoaji wanakukosoa, fanya tu jambo sahihi. Wana heshima kwako, chini ndani ya moyo wao. Na mimi niligundua hiyo kuwa ni kweli. Unaona? Basi kuwa mwaminifu na uwe mwadilifu. Watu wataheshimu hilo. Na hata ingawa wako makosani, wangali wanaliheshimu, unaona, kwa sababu ni—ni mwanadamu tu. Sisi sote ni wanadamu, na sisi—sisi tunajua kwamba kuna sahihi na lisilo sahihi, na sisi hatuna budi kuchukua hilo.

³⁷ Basi—basi Uzia alishikilia kiwango hiki. Alikuwa ni ushawishi mkubwa, kama nilivyosema, kwa Isaya nabii.

³⁸ Ndipo basi Uzia alifanya kosa hilo baya mno, kama vile tu watu wengine wengi hufanya. Wakati alipopata, alipojisikia salama, alijisikia kwamba alikuwa tu na kitu chote mkononi mwake, aliinuliwa rohoni mwake. Aliinuliwa, katika kiburi. Sasa huo hapo mfano halisi kwa ajili yetu sote.

³⁹ Mnajua, hiyo imekuwa ndiyo shida. Ni—ninazungumza na Wakristo na—na wahudumu, na ni—ninataka kuwa mwaminifu kuhusu mambo haya. Na hapo tu ndipo wahudumu wengi hata hufanya kosa. Tumesikia mara nyingi sana kuhusu wahudumu, ma—matendo wanayotenda, na—na kadhalika, baadhi yao labda kwa kufanya mambo wasiyoipaswa kufanya. Nafikiri wakati mwingine, wao ni watu wema, Wakristo wa ajabu ambao wametumiwa na Bwana. Na halafu hatimaye wanafanya ufalme mdogo kujengwa kuwazunguka, ama ushawishi mwingi, watu wengi wanahudhuria mikutano yao, mpaka wanakuwa wasiojali, na kwa namna fulani wanainuliwa. Watu wanawashangilia na kusimama, na—na sisi—sisi kwa kweli hatupaswi kufanya hivyo. Sisi, kumbukeni, sisi sote ni ninii tu. . .

⁴⁰ Hakuna watu wakubwa miongoni mwetu. Sisi ni—sisi sote ni watoto wa Mungu tu, unaona, kama Mungu alifanya baadhi yetu kitu kimoja na wengine kingine. Mbona, Yeye aliniumba nikiwa na kidole na jicho, na kadhalika. Vema, inatubidi kuthaminiana mmoja na mwenzake, na halafu tusijaribu kujisikia wakubwa. Kwa sababu, sisi sote tumeunganishwa pamoja na Mungu mmoja, unaona, na sisi sote tunatokana na mti mmoja. Unaona?

⁴¹ Na sasa tunakuta kwamba, mara nyingi, wahudumu hufikia kujisikia tu salama kidogo, na wanaendelea kuongoza huko, na, muda si muda mwajua, watafanya mambo ambayo hawapaswi kufanya. Na tunajua kwamba, mara nyingi, watu wenye haki na wazuri watafikia hata watakuwa na shughuli nyingi za kijamii kupita kiasi, wanataka tu kwenda nje kwenye sherehe kubwa, na, jambo la kwanza unajua, wataitisha kinywaji kidogo, mara moja moja, na wanaswa na ulimwengu. Na ninafikiri hiyo

ndiyo shida ya makanisa yetu leo. Nafikiri hiyo ndiyo shida ya huduma yetu ya Kipentekoste.

⁴² Sasa hebu nitaje hili kwanza, wazi. Unaona? Mnanisikia nikisema mambo kuhusu kanisa la Kipentekoste. Na mimi ni mpentekoste. Unaona? Bali, hapa, vipi kama hakukuwa na watu wa kipentekoste katika New York, usiku wa leo, ningeenda wapi kuhubiri Ujumbe huu? Unaona? Ninathamini watu wa Kipentekoste. Hao ni ndugu zangu na dada.

⁴³ Lakini hata hivyo wakati ninapoonza kitu kibaya na ndugu yangu, mtoto wangu, ama pengine mke wangu, ama chochote kilichokuwa, sahihi ni sahihi. Mzazi sahihi atasahihisha watoto wao.

⁴⁴ Na ninafikiri kwamba shida ya kanisa letu, tunajaribu sana kuwa kama we—wengine kupita kiasi. Unaona? Tunajaribu kutenda kama mtu mwingine, unaona, na—na tunaanza kuchukua tabia zao. Basi jambo la kwanza unajua, ilikuwa kwamba...

⁴⁵ Sikumbuki watu wa Kipentekoste mwanzoni mwao, bila shaka, wamekuwa ni miaka mingi iliyopita, katika huduma hii ya mwisho kutoka Barabara ya Azusa, bali nilichukua historia yake. Pia ni—nimesoma vitabu vingi, na kuzungumza na baadhi ya wazee. Ninatayarisha kuwa na mkutano sasa hivi pamoja na mmoja kule Shreveport, Louisiana, atakuwepo, alikuwa ni mmoja wa watu wa kwanza katika Barabara ya Azusa. Ndipo basi huo ndio mwanzo wa pentekoste katika nchi hii, yapata miaka hamsini na kitu iliyopita, nadhani. Nilihubiri yubile adhimu kwenye hekalu la McPherson, Hekalu la Angelus huko Los Angeles, miaka michache iliyopita, yubile adhimu ya mwaka wa hamsini wa pentekoste, sasa, mnaona.

⁴⁶ Lakini tangu wakati huo, kumekuwa na mambo mengi sana madogo madogo yanayopenyeza kuingia kanisani, kwa sababu kanisa halina budi kuchangamana na ulimwengu kila siku. Sasa, na simaanishi ku—kurudi kwenye hili tena, kwa—kwa dada zetu, unaona, ndugu zetu. Mara nyingi, ilikuwa miaka mingi iliyopita, kwamba ilikuwa ni kosa (kwa kuwa kama nilivyosema hivi majuzi usiku) kwa dada zetu kukata nywele, zao. Lilikuwa ni ja—jambo la Kipentekoste, kwamba hawapaswi kufanya hilo na mambo hayo. Lakini ni kitu gani? Sasa tunaenda katika sehemu mbalimbali za nchi, na tunakuta dada zetu wa Kipentekoste wakiwa na hiyo mitindo ya kukata nywele kichwamaji, mwajua, mitindo mikubwa ya kukata nywele namna hiyo. Na unaweza kuwaambia kuhusu hilo. Nao wanatumia vipodozi. Wa—wanavaa nguo kama mwanaume.

⁴⁷ Na wewe unasema, “Sasa, Ndugu Branham, unawashambulia wanawake.”

48 Sasa ngoja kidogo, hebu niwashambulie wanaume. Ndu—ndugu ambaye atamruhusu mke wake kufanya hivyo, yeye si mtawala sana wa nyumba yake. Unaona? Unaona? Unaona?

49 Hupaswi kufanya hivyo. Lakini ni kitu gani? Tumechangamana na wengine, maskini mnyonge fulani aliingia kutoka seminari fulani au shule, na analo wazo tofauti kuhusu hilo. Bali kuna mfano mmoja tu mkamilifu, huo ni, kurudi moja kwa moja kwenye Biblia. Biblia inahukumu hiyo, unaona. Nalo si sahihi.

50 Na ndipo tunapata vitu vingine. Ilikuwa ni kosa kwa watu wa utakatifu kuhudhuria sinema au filamu, mwajua. Sasa wanaenda wakati wote. Unaona? Na ndipo Shetani alivuta moja ya haraka juu yenu, akaweka televisheni moja kwa moja nyumbani mwako, na, unaona, akaiweka hapo ndani. Lakini mambo haya yote, kwamba ilikuwa ni kosa.

51 Vema, ni kitu gani? Unaona, inakuja pole pole sana mpaka, kitu cha kwanza unajua, imekunasa tu. Ni kama mmea-tambaaji unaokua kukuzunguka. Sasa, kama utauweka huo mmea-tambaaji mbali na wewe, unaona, na udumu tu umefungwa kwa Yesu, kulizunguka Neno na ukae na Hilo, unaona, utakua ukinyooka. Huo umepinda na unakuvuta kukutoa barabarani. Kristo hukuvuta juu. Huo hukuvuta kando.

52 Na ndipo unamwona mwanamke mmoja, kama mke wa mhudumu, ama mhudumu, anaanza kufanya jambo fulani, kanisa lake lote litasema, “Vema, mchungaji wetu hufanya hilo. Mke wa mchungaji hufanya hilo. Kwa nini tusifanye hili?” Unaona, unamshawishi mtu fulani, na uwe na hakika kwamba unawashawishi vizuri, kuelekea barabara sahihi na mambo ya kufanya ambayo ni sahihi.

53 Sasa tunapata, wakati unapoinuliwa, papo hapo uko njiani mwako kuanguka, unaona, unapojikweza.

54 Basi tunakuta sasa kwamba huyu Uzia, alijikweza kwa sababu alijisikia salama, yote kila kitu kilichomzunguka. A—alikuwa na taifa lake, na lilitunzwa vizuri, na Mungu alikuwa amembariki. Naye alikuwa na mashamba makubwa ya mzabibu, na mifugo na kondoo, na—na migodi, na kila kitu tajiri. Na mataifa yote yalikuwa na amani naye. Kwa hiyo a—akainuliwa tu juu mpaka akafikiria kwamba angeweza tu kufanya chochote ambacho a—alitaka kufanya, na kiburi.

55 Aliinuliwa sana mpaka akajaribu kuchukua mahali pa mhudumu. Aliingia ndani ya hekalu, na kuchukua chetezo na kuenda madhabahuni. Basi wakati alipofanya hivyo, kuhani alikimbia kumfuata na kumwambia hapaswi kufanya hivyo. Ndipo wakati aliporekebisha, badala ya kuwa mnyenyekevu jinsi ambavyo angekuwa... Kabla hajainuliwa juu, angesema, “Hiyo ni kweli, sina ha—haki kufanya hili,” na angeipeleka chetezo huko chini ama kumkabidhi kuhani ambaye alikuwa

ni wa Haruni, aliyekusudiwa kufanya hivyo, aliyewekwa wakfu kwa ajili ya huduma hiyo pekee.

⁵⁶ Mimi husafiri sana pamoja na ha—hawa hapa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Wengi wao wameketi papa hapa sasa. Na inanibidi kuzungumza kwenye kiamshakinywa chao, Jumamosi, Jumamosi asubuhi kwenye ninii. . . Kitu gani? Statler Hotel, ninaamini ndivyo ilivyo. Walisema walikuwa tayari wameuza tikiti elfu moja na mia saba kwa ajili ya kiamshakinywa tayari.

⁵⁷ Kwa hiyo basi, si muda mrefu uliopita, nilikuwa nikizungumza nao. Na wao walikuwa wakiwaleta wafanyabiashara juu kwenye jukwaa, wakichukua fungu lao na kuhubiri Injili. Nikasema, “Hilo ni kosa.” Kwa kweli ni kosa. Ni vigumu vya kutosha kwetu sisi wahubiri kuidumisha Hiyo ikiwa imenyooka; achilia mbali kuchukua mfanyabiashara ambaye hajawekwa wakfu kwa kitu kama hicho, kwamba unaingiza mawazo madogo, na kadhalika. Ndipo nikasema, “Hupaswi kufanya hilo.”

⁵⁸ Kamwe usijaribu kuchukua mahali pa mtu mwingine. Mungu alikufanya kitu fulani, basi wewe dumu hicho. Hakika. Wewe bakia tu kile ulicho. Usijaribu kumuiga mwingine. Hicho ndicho daima huharibu karama ambazo Mungu hutuma ulimwenguni. Tunakuta uigaji mwingi sana wa kimwili, na tunakuta mtu fulani anayejaribu kuiga kufanana na yule mwingine.

⁵⁹ Kama walivyosema kuhusu wanawake wahudumu, wakati Bibi McPherson alipokuwa hai, na kila mwanamke mhudumu alivaa hayo mabawa kama alivyovaa, ama chochote kile kilichokuwa, na walikuwa na Biblia yao vile vile. Na kila kitu alichofanya, walifanya.

⁶⁰ Tunatambua tunao akina Billy Graham wengi sana leo hii! Lakini unaona, Mungu kamwe hakufanya ila Billy Graham mmoja. Hivyo tu. Yeye. . .

⁶¹ Na wewe ni muhimu tu kama Billy Graham, Oral Roberts, au yeyote wa watu hao maarufu. Wewe ni muhimu tu mpaka unapoondoka mahali pako, ndipo basi hufai kitu hata kidogo, wewe—wewe ni—wewe ni kikwazo kwa—kwa watu hawa, na wewe ni kikwazo kwako mwenyewe na Ufalme wa Mungu. Dumu mahali pako. Unaona? Dumu kile ambacho Mungu alikufanya, unaona, na ndipo utatenda sawa.

⁶² Kama Paulo, si kitu chochote kipya, Paulo alifundisha jambo lilo hilo, kasema, “Ikiwa mkono utaambia jicho, ‘kwa sababu mimi si jicho,’ ama sikio kuambia pua, ‘si—sitakuwa sikio tena, kwa sababu mimi si pua,’” ama kitu fulani. Wewe, huwezi kufanya hivyo. Unaona, wote unashikana pamoja na kusonga kama mwili mmoja mkubwa.

⁶³ Na sisi ni lazima tusijaribu kumwiga yeyote. Kuwa tu kile ulicho, unaona, na hivyo ndivyo Mungu alivyokuumba. Kamwe hukujiumba mwenyewe. Pia, kumbuka, kadiri ambavyo sisi wahudumu tungependa kuchukua mahali pa Billy Graham, hatuwezi kufanya hivyo, wala na Billy Graham kuchukua mahali petu. Unaona, sisi, kila mmoja ana jambo la kufanya. Maskini jamaa wa kawaida hapa ambaye huenda ni bawabu, maskini mwanamke ambaye huenda ni mke nyumbani, mhudumu mashuhuri kuliko wote juu ya uso wa dunia leo hii asingeweza kuchukua mahali pako. Wewe, Mungu alikuwa na kusudi katika kukufanya kile ulicho, basi wewe mtumikie tu Mungu katika njia hiyo ambayo Yeye alikuumba. Unaona? Na mimi nafikiri, kama tungefanya tu hilo, magurudumu yangezunguka kwa urahisi zaidi. Naam, yangezunguka, kama tungefanya hivyo, si kujikweza. Na tunaona, badala ya . . .

⁶⁴ Wakati mtu fulani anapomwambia mtu jambo fulani, Kimaandiko, na sisi tunaona kuwa ni sahihi, badala ya—ya kujaribu kujinyenyekeza wenyewe, useme tu, “Vema, sasa, ni—nimekuwa makosani. Nisamehe. Na si—sikukusudia . . . Si—sikujua hilo, kwa hiyo nitaacha tu kufanya hilo.” Vema, basi, badala ya kufanya hivyo, mara nyingi sana tunafanya kama Uzia alivyofanya; alijisikia kuwa alikuwa mkubwa kupita kiasi cha kushushwa, unaona, yeye alikuwa ni mfalme. Na mara nyingi nimeona wahudumu hivyo, waliohisi kwamba walikuwa ni muhimu sana hata wasingeweza kuambiwa kile Neno lilicho, Kweli.

“Vema, siku za miujiza zimepita!”

⁶⁵ Ninaweza kukuonyesha mahali Mungu alipoweka miujiza; sasa wewe huwezi kuniambia mahali Yeye alipowahi kuiondolea mbali. Unaona? Na Yeye alikusudia karama; wewe hukuwahi kuona mahali Yeye alipoziondolea mbali. Unaona, iko katika Maandiko. “Enendeni ulimwenguni kote, hubirini Injili kwa kila kiumbe.” Kwa muda gani? “Ulimwenguni kote, mpaka kila kiumbe kiisikie, wote watakaoisikia. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Unaona, hatuwezi kuweka kitu chochote kingine badala yake. Chukua tu kile Yeye alichosema, na kitakuwa sawa na kitafanya kazi vizuri. Bali mradi tu tunajaribu kuchukua njia zetu wenyewe. . .

⁶⁶ Hapo ndipo Israeli ilipofanya kosa lao la kipumbavu kuliko yote. Wakati, neema ilikuwa imewapatia Nguzo ya Moto, Malaika, dhabihu, na kuwakomboa, ikawapelekea nabii, ikawapelekea Nguzo ya Moto kuwafuata, kumwongoza nabii njiani. Basi wakati walipofikia, Kutoka mlango wa 19, wakati walipobadilisha neema na torati, walifanya jambo la kipumbavu kuliko yote waliyowahi kufanya. Unaona? Lakini walitaka kitu fulani ambacho waliweza kufanya wenyewe.

⁶⁷ Hivyo ndivyo tulivyo sisi. Inatubidi kuwa na shahada yetu ya udaktari. Na kama hujaipata, huwezi kuingia kanisani. Hivyo tu. Kwa hiyo, na hatuna budi kuchunguza kitu hicho na kuona kama ni cha Mungu.

⁶⁸ Sasa tunaona, Uzia alijiinua, naye anaenda kuifanya hata hivyo. Alinyakua chetezo na kuondoka. Haikuleta tofauti yoyote kile makuhani walichosema, alikuwa anaenda kuingia kwa vyovyote vile! Na ilikuwa ni kinyume na Maandiko. Halikuwa jambo la kimaandiko kwake kufanya hilo.

⁶⁹ Si jambo la kimaandiko kwako wewe au mimi kumwiga yeyote mwingine. Kweli. Kwa hiyo kuwa kile ulicho, na uwe mzuri, na utimize kusudi lako ili wengine waweze kukuona. Kama wewe ni mke nyumbani, kuwa wa halisi, unaona. Kama wewe ni mu—mume, kuwa wa kweli, unaona. Na kama wewe ni shemasi, kuwa wa kweli; ama mhubiri, chochote ulicho. Bali usijaribu kuchukua mahali pa mtu mwingine.

⁷⁰ Na basi wakati Neno linapokuika kushuka kwenye hili, usininii. . . Kama unajisikia umekemewa, basi tubu. Hayo ndiyo yote, ni kuwa sahihi. Hilo ndilo jambo pekee la kufanya.

⁷¹ Bali Uzia hakutaka kufanya hilo. Baada ya Mungu kumbariki jinsi alivyokuwa amembariki, na hata hivyo hakujisikia kwamba angeweza kufanya hilo. Alidhania alikuwa anaenda kuendelea, alifanye kwa vyovyote vile, kwa sababu alijihisi alikuwa salama. Lakini wakati alipokuwa katika. . . Kwa namna fulani ilimfanya kuwakasirikia watu hao, pia, ambao walikuwa wakimwambia Neno la Bwana.

⁷² Na wakati alipofanya hivyo, aliingia ndani upesi, kwa vyovyote vile, na tunaona ya kwamba usoni mwake ulikuja ukoma. Naye alikuwa mwenye ukoma hadi alipofariki. Alikuwa kamwe hangeweza kuenda kwenye nyumba ya Bwana tena. Alikufa, mwenye ukoma. Baada ya yeye kuona mkono wa Mungu, na jinsi ambavyo Mungu alishakuwa mwema sana kwake na kufanya mambo ambayo Yeye alikuwa amefanya; hata hivyo mtu huyo alikufa, akiwa ametengwa, mwenye ukoma.

⁷³ Sasa tunaweza kufanya hilo. Tumeona mambo mengi, bali kamwe usifikirie kwamba tuko salama sana hata Mungu hawezi kuweka hukumu juu yetu, unaona. Unaona?

⁷⁴ Kumbuka, usijaribu kumwiga mtu yeyote mwingine. Kuwa tu kile ulicho. Ikiwa Mungu alikufanya mpentekoste, wewe kuwa wa halisi, unaona. Kama—kama Mungu. . . Usikionee haya. Siaibiki kuwa mwanadamu. Siaibiki kuwa Mmarekani. Si—siaibiki kuwa mhudumu. Sioni aibu kwa Injili ninayohubiri. Kwa sababu. . .

⁷⁵ Ninajua wengi wao wanafikiri kwamba nimepoteza akili zangu. Hata maskini mama yangu mwenye haki, aliyefariki miaka michache iliyopita. Wakati nilipopokea Roho Mtakatifu kwa mara ya kwanza, hakukuwa na mtu yeyote katika nchi yetu

aliyejua chochote kuhusu Huyo. Na mimi nilikuwa tu ni maskini, mhubiri kijana wa Kibaptisti, wa mahali hapo, yapata umri wa miaka ishirini. Lakini wakati nilipopokea Roho Mtakatifu, mama yangu alisema, “Mvulana huyo amerukwa akili.” Unaona? Lakini haijalishi kile mama alichofikiria, nilikuwa nimepata Lulu hiyo yenye thamani kubwa. Huenda ilionekana hivyo kwake yeye, bali kwangu mimi Hiyo ilikuwa halisi. Unaona, Hiyo ilikuwa. Ilikuwa ni kitu fulani cha kweli ambacho—ambacho nilikuwa nimepata katika Mungu.

⁷⁶ Kwa sababu, daima niliamini, kama mvulana, kwamba hili lilikuwa ni Neno la Mungu, na Hilo lisingeweza kubadilika. Yesu alisema, “Mbingu na nchi zitapita, bali Maneno Yangu hayatabadilika kamwe. Hayatapita kamwe.” Huwezi kubadilisha Hilo na chochote. Liko tu jinsi Hilo lilivyoandikwa, na hivyo ndivyo tunavyoliamini Hilo. Usiongeze chochote, wala kuondoa chochote Kwake. Unajua, huko katika Kitabu cha Ufunuo, Hilo lilisema, “Yeyote atakayeongeza neno moja, au kuondoa chochote kutoka kwenye Kitabu hiki, (kitu gani?) laana itakuwa juu yake.” Kwa hiyo liache tu jinsi Hilo lilivyo, na uamini Hilo namna hiyo, na Mungu ataliheshimu.

⁷⁷ Sasa yeye alipigwa kwa sababu ya kuinuliwa kwake kwa kiburi. Alipata hisia kwamba kulikuwa na . . . alikuwa ndiye wa pekee aliyekuwepo, na yeye angeweza kufanya kile alichotaka na hakuna yeyote mwingine angaliweza kumkomesha.

⁷⁸ Tulikuwa na ndugu, si muda mrefu uliopita, ambaye nilimhurumia sana. Ilionekana kana kwamba kila mtu alimlalamikia. Walimlaumu ndugu huyo kwa kufanya kosa fulani, ambalo gazeti lilililaumu. Bali ni—nilianza kuwaza kuhusu hilo, *kumlaumu* mtu huyo? Nilimtetea kwelikweli, maana . . . Kwa—kwa kweli sikukubaliana na yeye. Bali mtu yule aliyeandika makala na kuweka kwenye jarida, kwamba mtu huyu alikuwa amesema mambo haya yote mbalimbali na kufanya mambo haya.

⁷⁹ Ndipo usiku mmoja kwenye mkutano huko—huko Minneapolis, waliniambia kwamba mwandishi wa jarida hili alikuwepo. Na makala yalikuwa ndiyo kwanza yatokee kupitia jarida la Kikristo, kwa hiyo mimi . . . Ulikuwa ni muhtasari wa Kikristo. Kwa hiyo mimi . . . Wao, walinionyesha mtu huyo, mimi, kasema, “Ndiye yule aliyeketi *pale*.” Na yeye alikuwa katika makala haya, ambapo mhudumu huyu alikuwa ameandika jambo fulani, kitabu ambacho mtu huyo hakuandika. Ninakijua. Mama fulani alikiandika kitabu hicho, na mimi nilimjua mama huyo. *Kuuma Kwa Mashetani*.

⁸⁰ Kwa hiyo ni—nikasema, “Vema, sasa, jambo moja ambalo ningesema. Sasa, huenda nisikubaliane na huyo mhudumu, bali nafikiri, ikiwa nanii—ikiwa mhariri wa makala haya, ikiwa hakuyakagua maandishi yake vizuri si zaidi ya kusema

kwamba mtu huyu aliandika makala haya, na mimi ninajua yeye hakuyaandika, unaona, basi ninahofia mambo mengi zaidi aliyosema kuhusu mhudumu huyu ni uwongo.” Ndipo basi nikasema hivi, “Afadhali nipatikane hata makosani, kwa kujaribu kumfanya mtu aoko, kuliko kujaribu kumzuia mtu anayejaribu kumfanya mtu aoko.” Naam.

⁸¹ Heri nichukue mahali pa mtu huyo, wakati wowote, kuliko kujaribu kukosoa au kurarulia mbali kile ambacho mtu fulani anakijenga, hata ingawa wao—wao walifanya kosa au kufanya jambo fulani lisilofaa. Kwa hiyo lazima tuwe waangalifu, tunashawishi wengine juu ya kile tunachofanya.

⁸² Ndipo wakati mtu huyu alipopigwa na huu ukoma, wakati alipoinuliwa kwa kiburi, hili lilikuwa somo kubwa kwa huyo nabii kijana. Aligundua, kwa hili kuwa somo kubwa kwake, kwamba Mungu humweka mtu Wake mahali pake. Unaona? Mtu hawezi kujiweka mwenyewe. Mungu humwagiza mtu Wake. Mungu hukufanya kile ulicho. Unaona? Na Mungu humwagiza mtu Wake, na yeye sharti asijaribu kuchukua mahali pa mwingine. Na hilo lilikuwa somo kwa Isaya, kwamba lazima asiweke macho yake juu ya wanadamu kwa ajili ya mfano. Lazima aweke macho yake juu ya Mungu.

⁸³ Sasa hiyo ni sisi. Mtu yeyote, mtu yeyote anaweza kufanya makosa. Anaweza kukosea kwa sababu ni mwanadamu. Anaweza kukiuka sheria za Mungu. Na yeye anaweza kupatwa na mambo mengi, kwa sababu Shetani humjaribu, na yeye ni mwanadamu tu. Basi ikiwa Mungu aliwahi kuinua mikono Yake, yeye angeanguka. Hivyo tu.

Na mimi nimesikia watu wakisema, “Loo, Shetani hawezi kufanya hilo.”

⁸⁴ Naam, acha Mungu ainue tu mkono Wake wakati mmoja, na uangalie kinachotendeka. Ni ninii. . . Daima ninasihi, “Mungu, usimtume. Nirehemu. Mweke mbali na mimi,” unaona. Ni—ninahitaji rehema ya Mungu. Na sisi sote tunahitaji hiyo.

⁸⁵ Sasa tunakuta kwamba, Isaya, alikuwa ameegemea pakubwa juu ya mkono wa mfalme aliye mwema, na sasa mkono huo ulikuwa umeondolewa kwake; naye mfalme alikufa, na alikufa kwa ukoma, katika aibu. Sasa, Isaya, kwenye wakati huu, mfalme akiinuliwa, vema, ndipo mwana wake kijana alikuwa achukue mahali pake. Na sisi tunaona kwamba—kwamba watu walikuwa wameingia katika ha—hatua ya kutisha ya utovu wa uadilifu.

⁸⁶ Wakati hakuna kiongozi halisi mtauwa, basi watu wanaanza kuingia katika utovu wa uadilifu. Nafikiri hiyo ndiyo shida tuliyo nayo leo hii, katika taifa letu, katika makanisa yetu, na kadhalika. Tunahitaji viongozi watauwa, mtu ambaye anaweke mfano.

⁸⁷ Na, bali Yeye alimruhusu Isaya kujua hapa kwamba asingeweza kuwatumainia wanadamu. Kwa hiyo Isaya, siku moja, alipokuwa anazunguka kote, hapana shaka alikuwa mchovu sana, kwa kuwa alijua alikuwa na jukumu kubwa, alishuka kwenda hekaluni kuomba. Sasa hilo ni jambo jema kufanya, kwetu sote. Anashuka kwenda hekaluni kuomba.

⁸⁸ Basi tunatambua wakati alipokuwa anaomba huko chini madhabahuni. Mara ghafla, akiwa ni nabii, aliingia katika ono. Ndipo, wakati alipoingia, alitazama juu na akamwona Mungu, Mfalme, akiwa ameketi juu kabisa, ameinuliwa, juu kwenye kiti Chake cha enzi, na vazi Lake likajaza mahali hapo, unaona. Ndipo akaona mfano halisi. Alimwona Mmoja ambaye angeweza kumtumainia, ambaye hangeweza kupigwa na ukoma, Mmoja ambaye hangeweza kushindwa. Kwa maneno mengine, Yeye alikuwa anamwambia Isaya, “Angalia, uliweka tumaini lako katika mwanadamu fulani, na lilishindwa. Uliweka ninii yako... ulimtazamia mtu huyu kwa ajili ya mfano, na—naye akashindwa. Sasa tazama juu Hapa, kwangu Mimi, Mimi ndimi Mungu asiyeshindwa.”

⁸⁹ Nami na—nafikiri hilo ndilo tunalopaswa kufanya leo hii, kama watumishi Wake, tunapaswa kumtazama Yeye. Yesu ndiye mfano wetu. Na sisi hatuna budi kumtazama Yeye, Mbuni na Mwenye kukamilisha imani yetu.

⁹⁰ Sasa tunaona, katika ono hili, kwamba alimwona Mungu ameinuliwa juu kwenye kiti cha enzi. Ndipo akaona kitu kingine. Tazama, kumzunguka walikuwa, na ndani ya hekalu mahali Yeye alipokuwa, walikuwa hawa Maserafi wa Kimbinguni.

⁹¹ Kama ungechunguza neno hilo, nafikiri linatumika tu mara moja ama mara mbili katika Biblia. Na si—si Makerubi, bali ni wa pili kutoka kwa Makerubi. Kitu kama Kiumbe cha Kimalaika; na hata hivyo si Malaika, na ni Malaika, bali ni Mtu spesheli. Kile Hao walicho, Hao ni wateketezaji sadaka, katika Biblia. Na mahali ambapo sadaka, bila shaka, huingiza au huongoza katika... hufanya njia kwa ajili ya mwenye dhambi, kwa utakatifu. Na hawa Maserafi wakiteketeza dhabihu iliyohitajika, Wao—Wao walienda kwenye... Hilo lilikuwa ni jukumu Lao.

⁹² Na walikuwa ni Hao hapo, wakiruka kupitia hekaluni wakati Isaya alikuwa katika ono, na hekalu lote likajaa moshi. Na Wao walikuwa wakiitana, Mmoja na Mwenzake, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi! Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu!” Loo, kwa maneno mengine, “Kuna Kitu fulani ambacho hakiwezi kuanguka. Huo hapo mfano wako. Huyu hapo Mfalme wa kutazamia. Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi!”

⁹³ Na tunakuta sasa kwamba hawa walikuwa ni viumbe wenye mabawa sita. Na sasa tunaenda kuchunguza sababu ya kuwa na

mabawa sita. Walikuwa na, tunaona, Wao walikuwa na mawili juu ya uso Wao, mawili juu ya miguu Yao, na walikuwa wanaruka kwa mabawa mawili.

⁹⁴ Sasa angalia, kwanza, kwamba viumbe hawa walikuwa wanahudumu katika Uwepo wa Mungu. Na huo ulikuwa ni wajibu Wao, walikuwa wakilia, “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi!” Na Wao wakalia, mchana na usiku, katika Uwepo Wake, huku dhabihu imewekwa pale. “Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana Mungu Mwenyezi!”

⁹⁵ Na ninawatakeni mwone kitu fulani hapa, na mwazie. Hao Maserafi walikuwa na mabawa mawili juu ya nyuso Zao. Ni kwa nini Wao waliweka hayo juu ya nyuso Zao? Kwa sababu Wao walikuwa katika Uwepo wa Mungu. Basi wazia tu, ikiwa Malaika watakatifu inabidi wafunike uso Wao, katika Uwepo Wake, vipi kutuhusu sisi? Wana mabawa juu ya nyuso Zao, iliwakilisha kicho.

⁹⁶ Lakini, leo hii, tunakuta kwamba hakuna uchaji wowote. Ni vigumu kupata uchaji. Hawana heshima yoyote kwa Mungu. Wanasimama na kuimba *Mungu Ibariki Marekani*, huku mguu wao ukiwa kwenye baa. Na ni la kutisha mno, jinsi wanavyofanya.

⁹⁷ Nilienda kuomba sandiwichi, leo hii, ma—mahali fulani. Na maskini mama huyo, si kutoa matamshi yoyote kumhusu, bali nilifikiria alikuwa anakufa. Alionekana kana kwamba alikuwa ameoza chini ya macho yake, alikuwa na samawati kote mwilini mwake. Ndipo—ndipo akakimbia, akiwa amevalia tu nguo chache, na akasema, “Utakula nini?”

⁹⁸ Nikasema, “Waweza kuniletea sandiwichi na bi—bi—bi—bi—bilauri ya mtindi wa maziwa?”

Naye akasema, “Bourbon” juu ya kitu fulani, namna fulani.

⁹⁹ Nikasema, “La, mama. Ulinielewa vibaya.” Nikasema, “Nilisema, ‘mtindi wa maziwa.’”

Naye akasema, “Loo,” kasema, “hutahitaji kinywaji chochote?”

Nikasema, “Ninataka mtindi wa maziwa.”

¹⁰⁰ Ndipo akasema, “Vema, nyinyi nyote, hivi hutaki. . . Wakati wa usiku sisi huandaa *ninii*.”

Nikasema, “Mimi ni mhudumu.”

¹⁰¹ Akasema, “Vema, nanii wetu. . . Vema, makasisi wetu wa Katoliki huja hapa na kunywa.”

¹⁰² Nikasema, “Mimi—mimi si kasisi wa Katoliki, mama. Ni—ninataka. . . Ninataka bilauri ya mtindi wa maziwa.” Ilionekana kana kwamba ilimshtua mwanamke huyo. Hakujua ulikuwa ni kitu gani. Unaona?

¹⁰³ Na ulimwengu umefikia mahali kama hapo. Sasa kama kasisi anaingia na kunywa, kusanyiko lina haki kunywa; huo hapo mfano wako, unaona. Loo, jamani, ni uozo wa jinsi gani tunaishi ndani yake! Tunahitaji kusafishwa kwa nyumba, kote kote kuanzia mimbarani hadi kwenye. . . Naam. Naam, bwana, hakika tunahitaji. Jinsi uozo wa ulimwengu!

¹⁰⁴ Na hawa, hakuna kicho, hakuna heshima! Watu leo hii, hawamheshimu Mungu. Hawana kicho. Wanataja Jina Lake bure, na kutoa mizaha michafu. Na—na hata wahudumu hufanya hivyo. Ukisikia m—mzaha, nadhani itakuwa sawa. Bali wahudumu wanapaswa kuwa mifano, nafikiri, ya kile ya—ya haki na utakatifu. Na hiyo ndiyo sababu nafikiri labda hatu—hatufiki mbali kuliko tufanyavyo; hatufiki, hatufikii huu, uaminifu tunaopaswa kuwa nao katika hilo. Wakati unapofanya yasiyofaa, na kuendelea, unapoteza chembe hiyo ndogo ya uaminifu, unajua. Kuna jambo fulani kuhusu hilo.

¹⁰⁵ Lazima ukumbuke kwamba Mungu anakuona, kila saa. Yeye hukuona wakati umelala. Sasa, nafikiri sababu ya watu kufanya mambo hayo ni kwa sababu, wao—wao—wao, hawautambui Uwepo Wake, unaona. Lakini hata hivyo Yeye yupo, kama unafikiria kuwa Yeye yupo au la. Yeye huona kila mtazamo unaofanya, na kila—kila msogeo unaofanya. Anajua yote kuuhusu. Bali tunapaswa kutambua hilo.

¹⁰⁶ Tulikuwa na wimbo mdogo, wakati nilipokuja miongoni mwa Wapentekoste kwa mara ya kwanza, waliimba.

Kote barabarani kuelekea kwenye makao ya
kweli ya nafsi,
Lipo Jicho linalokuangalia;
Kila hatua unayopiga, Jicho hili kuu liko
macho,
Lipo Jicho linalokuangalia.

Mnaona? Je! mnakumbuka wimbo huo? [Kusanyiko linasema, “Naam.”—Mh.] Sasa hiyo ni kweli.

¹⁰⁷ Uwepo wa Mungu kila mahali unajua kile unachofanya, na hata mawazo yako. Wakati mmoja nilipokuwa katika ono, nilikuwa nikizungumza na Kiumbe kilichosimama karibu na mimi; na Yeye akasema huko nyuma, Yeye akasema, “Mawazo yako yana sauti kubwa zaidi Mbinguni kuliko sauti yako ilivyo duniani.” Anajua kile unachowazia. Huenda ukasema wewe—wewe hufanya *hili* na wewe hufanya *lile*, na *hicho*, bali, unaona, chini ndani ya moyo wako, kama unafikiria tofauti, una—unafanya kosa. Unapaswa kuwa tu kile ulicho, unaona, mo—moyo. Kinywa kinapaswa kunena yaliyoko ndani ya moyo. Unaona? Na kwa hiyo tunaona kwamba watu hawatambui U—Uwepo wa Mungu.

¹⁰⁸ Unajua, wanapaswa kuwa kama Daudi, mtu aliyeupendeza moyo wa Mungu Mwenyewe. Alisema, “Bwana daima yuko

mbele zangu.” Popote aendapo, yeye hukumbuka Mungu daima yuko mbele zake. “Yeye yuko kwenye mkono wangu wa kulia, basi sitatikisika,” kwa sababu Mungu yuko kwenye mkono wake wa kulia.

¹⁰⁹ Kicho! Tunapaswa kuheshimiana mmoja na mwenzake, kuheshimiana mmoja na mwenzake, kama ndugu, dada. Na kupendana mmoja na mwenzake, kwa upendo usiopungua. Unasema, “Vema, siwezi kabisa.” Vema, bakia tu *hapa* muda mrefu kidogo, na ndipo utawapenda watu, pia. Utawapenda wale wasiokupenda. Hiyo kweli ni ishara nzuri ya Ukristo: wakati unapoweza, kutoka moyoni mwako, kuwapenda wale ambao hawakupendi. Wapende wasiopendeke.

¹¹⁰ Yesu alisema, “Ukiwafanyia fadhili wale tu ambao hukufadhili, vema, watoza ushuru hufanya jambo lilo hilo.” Bali, unaona, lazima uwahurumie wale wasiokuhurumia. Watendee wema wale ambao wangekutendea uovu. Daima kumbuka hilo. Weka hilo mbele zako, kwamba Mungu anakutazama. Kumbuka, Mungu alikuwa mwema kwako wakati ulipokuwa mwovu Kwake. “Wakati mlipokuwa mngali wenye dhambi, Kristo alikufa kwa ajili yenu.”

¹¹¹ Sasa tunaona, kwamba, mabawa haya juu ya nyuso Zao yalikuwa ni kwa sababu Wao walikuwa katika Uwepo wa Mungu, wenye kicho. Na ikiwa Serafi mtakatifu inambidi kuficha uso Wake nyuma ya kifuniko maalum, Yule ambaye hajui dhambi yoyote, hakuwahi kutenda dhambi, lakini hata hivyo katika Uwepo wa Mungu Mtakatifu inambidi kufunika uso Wake mtakatifu katika Uwepo wa Mungu, mnaiki atafanya nini katika Siku hiyo? Aliyerudi nyuma atafanya nini katika Siku hiyo? Asiyemcha Mungu atafanya nini katika Siku hiyo, wakati utakapokuja? Na inaenda kukulazimu kukabiliana na Yeye.

¹¹² Lipo jambo moja tu. Unasema, “Lakini Yeye kamwe hakunitengenezea mabawa kufunika uso wangu.” Lakini Yeye alimwaga Damu ya Mwana Wake Mwenyewe, ili uweze kufunika uso wako kwa hiyo. Hiyo ni kweli. Hicho ndicho kifuniko Chake pekee alichacho Yeye kwa ajili ya jamii ya wanadamu, ni Damu ya Yesu Kristo.

¹¹³ Sasa, la pili, Wao walifunika miguu Yao kwa mabawa, chini ya miguu yao. Sasa hilo liliwakilisha unyenyekevu. Loo, hilo hapo neno ambalo limepotea leo hii, kwa watu wengi. Unyenyekevu katika Uwepo Wake. Kujinyenyekeza wenyewe katika Uwepo Wake.

¹¹⁴ Nimemwona Roho Mtakatifu akija katika chumba na—na kutimiza na kufanya mambo yale hasa ambayo Biblia ilisema Yeye angefanya, kupambanua, na nimeona watu wakiinuka na kutoka nje. Nimeona watu wakiketi na kuongea, na kucheka na kumdhihaki Huyu, wakati ilipokuwa inaendelea.

115 Ninakumbuka usiku mmoja, mhudumu aliwaleta ishirini na wanane wa kusanyiko lake, na walikuwa wameketi. Hii ilikuwa ni huko Jonesboro, Arkansas.

116 Nao walikuwa na mvulana mwenye kifafa, alikuwa na kifafa. Na hicho ni ibilisi. Ni ibilisi. Hicho ndicho kilicho. Hawaninii, madaktari hawajui ni kitu gani hufanya hilo. Ni ninii—ni ibilisi. Nao waliweka ninii... walikuwa na kipini cha nguo pamoja na ki—ki—kitambara kimefungwa kukizunguka; alipokuwa na vipindi hivi vya kifafa, wangekirusha kinywani mwa mvulana huyo, maana angetafuna ulimi wake basi. Ndipo wakamleta mvulana huyo, na—na alikuwa na kipindi hiki cha kifafa moja kwa moja jukwaani. Bila shaka, wakisimkwa kidogo, wataingia katika kimoja. Kwa hiyo wakati tulipokuwa tukijiandaa kumwomba mvulana huyo, nilisema, “Hivi kila mtu atainamisha vichwa vyao kwa kicho?” Na ni—nikamwomba, na ro—roho huyo asingemwacha mvulana huyo.

117 Nami nikaangalia kote, na nikaona kundi dogo limeketi mahali fulani. Nikasema, “Waweza kuinamisha kichwa chako?” Nikasema, “Lazima utii.” Nikasema, “Hilo lilikuwa ndilo agizo, ‘Ukiwafanya watu wakuamini, na halafu uwe mwaminifu unapoomba.’” Nikasema, “Waweza kuinamisha kichwa chako?” Jamaa huyo akanicheka tu.

118 Na kwa hiyo nikageuka, lakini, huyu, asingemwacha mvulana huyo. Na sasa haya yalikuwa ni mamia ya watu, mara tano ya wale wanaoketi hapa usiku wa leo, wameketi huko, naam, mara nyingi. Walidai kulikuwa na watu elfu ishirini na nane huko. Kwa hiyo—kwa hiyo kulikuwa—kulikuwa, wote walikuwa...

119 Ndipo basi nikasema, “Ni—nisingefanya hivyo, bwana.” Na yeye alikuwa ni mshiriki wa ka—kanisa la kidhehebu ambalo kwa urahisi lilicheka tu uponyaji wa Kiungu, hawaamini kuna kitu kama hicho.

120 Kwa hiyo nikaangalia kote. Maskini mvulana huyo, koo lake limetokeza. Huku mama yake akijaribu kupiga mayowe, mama akilia namna hiyo. Naye mvulana huyo akijaribu kumeza, na kuendelea.

121 Nikasema, “Baba wa Mbinguni, usimwache mvulana huyu asiye na hatia kuteseka kwa ajili ya kundi hilo lenye hatia, unaona.” Nikasema, “Hilo lilikuwa ni Neno Lako—Lako, na mimi—mimi nimekuwa mwaminifu na kuwaambia. Na wengi sana wenye kifafa wameponywa hapa kwenye mkutano.” Nikasema, “Usimwache mvulana huyu asiye na hatia kuteseka. Mama na baba walimleta hapa. Ninaomba kwa ajili ya rehema.”

122 Ndipo nikageuka, nikasema, “Katika Jina la Bwana Yesu, kwa imani, kwa agizo langu nililopewa na Mungu Mwenyezi, ibilisi huyu hawezi kumshikilia mvulana huyu. Uko

huru, unaona. Kama wasiotii watakosa kutii, basi uko huru kuwaendea, lakini toka ndani ya mvulana huyo.”

¹²³ Na nikaona watu ishirini na wanane, pamoja na mchungaji wao, wakianguka katika kifafa, moja kwa moja kuzunguka na kuzunguka, na kuzunguka na kuzunguka, sakafuni namna hiyo. Na kadiri nijuavyo, wangali wanacho, unaona.

¹²⁴ Sasa, unaona, lazima msiwe wasio na kicho. Lazima mjinyenyekeze. Ni wangapi wenu wamekuwa katika mikutano na kuona mambo kama hayo yakitendeka katika mikutano yangu? Ninii tu, mbona, unaona. Hakika. Naam, bwana.

¹²⁵ Wakati mmoja walimleta mtu kunipumbaza akili. Nadhani wengi wenu mnakumbuka hilo. Na wao—wao wangemtoa kumpeleka kwenye makambi ya kijeshi, na—na kuchukua askari hawa na kuwapumbaza akili, kuwafanya wabweke kama mbwa. Na wao walikuwa wanaenda kupata mchezo fulani kutoka kwangu. Kwa hiyo nilikuwa katika ukumbi, nao wakamleta mtu huyu. Na—nami nikahisi, wakati mstari wa maombi ulipoanza, kulikuwa na roho mwovu mahali fulani.

¹²⁶ Daima unaweza kuwatambua wao na shaka hilo. Wanafikiria hawatilii shaka. Ilikuwa. Unaweza kulihisi. Ni tofauti.

¹²⁷ Kwa hiyo basi ningeweza kusema lilikuwa wapi, bali nisingeweza tu kuona mahali mtu huyo alipokuwa. Baada ya kitambo, nililipata na nikaona kile lilichokuwa. Niliona giza hilo likining’inia juu yake. Na sikutaka kusema hilo, bali nilimgeukia tu mtu huyo, nikasema, “Mtoto wa ibilisi,” unaona, “ni kwa nini ibilisi ameweka niani mwako kufanya hilo? Kwa sababu amefanya hilo,” Kitu fulani kilikuwa kinalisema ndani yangu, “watakubeba kutoka hapa.” Na angali amepooza. Unaona?

Barua baada ya barua, “Njoo kwake!”

¹²⁸ Nikasema, “Jambo pekee nijualo, ni kutubu. Unaona, kamwe sikufanya hilo. Hiyo ilikuwa ni kukosa kwako kicho mbele za Mungu.” Unaona? Sasa usifanye hivyo. Sisi ni. . .

¹²⁹ Tumekuja nyakati ambazo watu hufikiria kwamba utakatifu huu mbele za Mungu ni namna fulani tu ya dhihaka, ama namna fulani ya ku—kundi la watu ambao hawajui, namna fulani ya dini potovu au ukoo, au kitu fulani. Lakini hebu nikuhakikishie, ndugu! Huenda kukawa na dhihaka nyingi. Si—sisemi kwamba hakuna; si—si—siwezi kusema hivyo. Mimi ni mwanadamu tu. Sipaswi kuhukumu. Ninapaswa tu kuhubiri. Bali kuna Roho Mtakatifu halisi, Nguvu halisi za kimitume za Roho Mtakatifu. Na katika nchi za kigeni, na wachawi na kadhalika huinuka, hao pepo, kupiga vita. Loo, kama tungeninii tu. . . Ngingekatiza somo langu hapa, kuenda kuwaambieni kuhusu mambo hayo. Na kitu gani? Roho Mtakatifu, kamwe hata wakati mmoja sijawahi kumwona Huyo akishindwa kufanya hilo. Atalifanya kila wakati.

¹³⁰ Tazama sasa, waliweka, walikuwa na mabawa juu ya miguu yao kwa ajili ya unyenyekevu. Hatupendi kujiinamisha. Tunataka kufikiria kwamba sisi ni mtu fulani.

¹³¹ Ninakumbuka hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa kwenye maskini jumba la makumbusho, na—na wao walikuwa na u—uchambuzi wa mwanadamu mwenye uzito wa ratili mia moja na hamsini, nini thamani ya mwili wake katika kemikali. Ninaamini ilikuwa senti themanini na nne, mtu mwenye uzito wa ratili mia moja na hamsini, ke—kemikali zake za mwili wake. Alikuwa na kalishi kidogo, na chokaa ki—kidogo ya kutosha labda kunyunyizia kiota cha kuku, na kadhalika. Hayo karibu tu ndiyo yote a—aliyokuwa nayo ndani yake, mwenye uzito wa ratili mia moja na themanini na nne. . . ama ninamaanisha senti themanini na nne, mwenye uzito wa ratili mia moja na hamsini.

¹³² Kulikuwa na wavulana wawili waliosimama hapo, wakiangalia hili. Na mimi nilikuwa nimesimama moja kwa moja nyuma yao, huku mmoja wao alisema, “Vema,” kasema, “John, hatuna thamani kubwa hata hivyo, sivyo?” Naye akasema, “Nadhani hatuna.”

¹³³ Nami nikasema, “Vema, wavulana, hiyo ni kweli, unaona, hamna thamani kubwa sana katika kemikali. Bali unayo nafsi ndani yako, unaona, iliyo na thamani ya ulimwengu milioni moja, unaona.” Hiyo ni kweli. Unaona?

¹³⁴ Bali hata hivyo sisi—sisi tunataka kushughulikia, tuna kiburi ndani ya senti hizi themanini na nne, tunazifunga katika koti la bei kubwa ya dola mia tano, na—na kuinua pua yetu juu hewani, na kufikiria sisi—sisi tunafanya jambo fulani. Simaanishi kufanya mzaha. Huu si mzaha. Hii, hii ni kuwaambieni tu kile tulicho. Unaona, sisi ni—sisi ni—sisi ni. . .

¹³⁵ Hatuna unyenyekevu. Hatutaki, na watu hawataki. Unaenda wakati mwingine kwenye watu waliovalia nadhifu kwelikweli kanisani, wao—wao wataingia; na ikiwa wewe hujavalia tu vizuri, watakuangalia na kuongea, unajua. Na hiyo hufanya ninii yake. . . Hawapaswi kufanya hivyo, na kukiri Ukristo. Na—na—nafikiri ni maungamo tu wala si umiliki. Kwa sababu ninaamini kwamba u—uzoefu halisi wa mtindo wa kale na Mungu utafanya koti rasmi kuikumbatia jozi ya surupwenye, na kusema, “ndugu.” Ni—ninaamini hilo kabisa. Ni kweli. Gauni la kaniki na la hariri, ataita, “dada.” Naam, bwana. Kwa sababu, si nguo, si mtu huyo. Ni Kristo, kile kilichoko ndani, na sisi tunapaswa kujinyenyekeza.

¹³⁶ Sasa tunapata ya kwamba, ni, Malaika hawa walifunika miguu Yao, ama Maserafi hawa.

¹³⁷ Musa, wakati alipokuwa katika uwepo wa Mungu, ambaye, mwangalie kupitia hiyo Nguzo ya Moto iliyokuwa huko nyuma katika kile kichaka kilichowaka moto, Bwana alinena. Na yeyote anajua hiyo Nguzo ya Moto ilikuwa Kristo, Yeye alikuwa ndiye

Malaika wa Agano. “Musa aliacha Misri, akahesabu shutuma la Kristo kuwa hazina kubwa kuliko ile ya Misri.” Kwa hiyo, Hiyo ilikuwa ni Malaika wa Agano. Na wakati Yeye alipotokea katika kile kichaka kilichowaka moto pembeni, mbona, mbele za Musa, na Sauti ikasema, “Vua viatu vyako.” Miguu yako, unaona. “Vua viatu vyako, kwa kuwa mahali uliposimama ni patakatifu.” Musa alijinyenyekeza, kwa kuvua viatu vyake.

¹³⁸ Nguzo iyo hiyo ya Moto ilimtokea Paulo njiani akielekea Dameski, siku moja.

¹³⁹ Mnakumbuka, Yesu, wakati Yeye alipokuwa hapa duniani...Walisema, siku moja walisema kulikuwa na... Katika Yohana Mtakatifu 6, walikuwa wakinywa kutoka kwenye chemchemi, na kushangilia. Ndipo Yeye akasema, “Mimi, mimi ndimi Maji yale yatokayo kwenye ule Mwamba. Mimi ndimi Mkate wa Uzima uliotoka Mbinguni,” unaona, namna hiyo.

¹⁴⁰ Wasingeweza kuliadini hilo. Walisema, “Mbona, hapa! Tunajua Wewe una pepo, na Wewe ni mwendawazimu,” inamaanisha *mwenye kichaa*. “Kwa sababu, Wewe hujapita umri wa miaka hamsini, na Wewe wasema ati Wewe ulimwona Ibrahimu?”

Akasema, “Kabla Ibrahimu hajakuwako, MIMI NIKO. Naam, MIMI NIKO.”

¹⁴¹ Sasa tunaona hilo, kwamba Yesu alisema, “Nalitoka kwa Mungu. Ninaenda kwa Mungu.” Wakati Nguzo hii ya Moto ilipofanyika mwili, Mungu akija kutoka kwenye Ubaba, [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]...Uwana, na wakati Yeye alipokuja ndani ya sifa hii. Sifa hizo tatu; Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu. Wakati Mungu alipodhihirishwa katika mwili, Yeye alisema, “Nimetoka kwa Mungu. Na ninaenda kwa Mungu,” ndipo Yeye akapaa juu.

¹⁴² Na—naye Sauli wa Tarso, njiani mwake akielekea Dameski, aliangukwa chini na Nuru. Na wakati alipoanguka, alitazama juu. Na huyo Myahudi asingaliweza kuita chochote “Bwana” kama Hiyo haikuwa ile Nguzo ya Moto. Aliiona Nuru hiyo pale, ndipo yeye akasema, “Bwana, U Nani Wewe?”

Yeye akasema, “Sauli, ni vigumu kwako kupiga teke vichokoo.”

Na yeye akasema, “U Nani Wewe, Bwana?”

Yeye akasema, “Mimi ni Yesu.” Unaona, ile Nguzo ya Moto tena.

¹⁴³ Mwangelie Sauli, alijinyenyekeza katika vumbi, unaona, katika Uwepo wa Mungu. Unyenyekevu! Amepigwa akaanguka chini, amelala kwa mgongo wake labda, akitazama juu.

¹⁴⁴ Ndipo ile Nguzo ya Moto ikizunguka pale, yeye aliona na kujua. Kama mwalimu kutoka chini ya Gamalieli, mwalimu mashuhuri wa siku hiyo, alijua kwamba Mungu alikuwa

amewaongoza watu Wake katika umbo la Nguzo ya Moto. Na Moto huo, Nguzo ya Moto, ilikuwa imefanyika mwili na kukaa miongoni mwao, na alikuwa amesulubiwa kwa ajili ya dhambi zao, “na mimi natoka kwa Mungu; na ninarudi kwa Mungu,” na alikuwa Huyu hapa, bado katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁴⁵ Na ndipo tunakuta basi katika hilo, baadaye kabla tu ya hapo, Yohana Mbatizaji, mkuu kuliko manabii wote. Manabii wote walinena kuhusu Yeye kuja; Yohana alisema, “Huyu Ndiye.” Yeye, alimtambulisha Yeye kwa ulimwengu. Na Yohana akisimama pale kwenye maji, wakati alipokuwa akibatiza, na yeye—yeye alikuwa akisema, “Kunakuja wakati ambapo dhahibu za kila siku zitaondolewa hekaluni, na kutakuwa na Mtu atakayekuwa dhahibu.” Na Yohana alikuwa na hakika kwamba alikuwa anaenda kumwona Masihi.

¹⁴⁶ Unaona, wakati Yohana alipoitwa, baba yake alikuwa ni kuhani. Bali kwa kawaida mvulana alifuata, katika siku hizo, na wanafanya kule Mashariki bado, kazi ya baba yake. Na kwa kawaida yeye angekuwa kuhani. Lakini Yohana kamwe hakuenda kwenye shule hiyo. Maana, Yohana alizaliwa, kutoka tumboni mwa mama yake, “amejawa Roho Mtakatifu.”

¹⁴⁷ Wakati, Elisabeti alipokuwa ameshika mimba na mtoto alikuwa amekufa tumboni mwake. Wakati Mariamu alipozuriwa na Malaika, Gabrieli, na kumwambia kwamba binamu yake Elisabeti, aliyekuwa amepita umri wa kuzaa, pia angepata mimba. Ndipo Mariamu akakimbia kwenda kukutana naye. Na yeye alikuwa amejificha, na alikuwa na wasiwasi kwa sababu mtoto hakuwa amecheza kwa miezi sita, na hiyo si kawaida. Na kwa hiyo alimwona Mariamu akija, akatoka mbio na kumlaki, na kumkumbatia. Naye akasema, akaanza kuongea. Na—na yeye akasema, “Ninajua alikuwa anaenda kuwa mama.” Akasema, “Ndiyo, na mimi—mimi ninaenda kuwa mama, pia.”

“Loo, nadhani wewe na Yusufu mmefunga ndoa.”

“La, la. Hatujafunga ndoa bado.”

“Na wewe ni mja mzito?”

¹⁴⁸ “Ndiyo. Roho Mtakatifu alinitia uvuli, na kusema kwamba Kitu hicho Kitakatifu kitakachozaliwa nami, ndani yangu, kitakuwa ni Mwana wa Mungu, na ninapaswa kumwita Jina Lake ‘Yesu.’”

¹⁴⁹ Na punde tu Neno hilo “Yesu” lilipotamkwa mara ya kwanza kutoka kwenye mdomo wa bidanadamu, mtoto ambaye hakuwa amewahi kuwa na uhai ndani yake, bado, alipokea uhai ndani ya tumbo la mama yake na kuanza kuruka kwa furaha. Na kama Jina la “Yesu Kristo” litaleta uhai kwa mtoto aliyekufa, Hilo linapaswa kufanya nini kwa kanisa lililozaliwa upya ambalo hudai kujazwa na Roho Mtakatifu? Unaona?

150 Sasa huyu anapaswa kuwa ni mvulana wa aina gani? Alikuwa amtangaze Masihi ajaye. Malaki 3 ilisema angemtangaza. “Tazameni, namtuma mjumbe Wangu mbele ya uso Wangu.”

151 Sasa, kama angeenda huko chini kwenye seminari, baadhi ya hao wahudumu huko chini, kasema, “Sasa, Yohana, wewe unapaswa kumtangaza Masihi, mbona, wewe—wewe unajua kwamba Uncle Joe hapa, ama—ama—ama Baba Jim, ama baadhi yao, unajua yeye anazo si—si—si—sifa zote za kuwa Masihi, huyo ni yeye, Yohana,” ambaye—ambaye... unaona, angalishawishiwa na wanadamu.

152 Alienda nyikani, naye alikaa pamoja na Mungu. Hiyo ndiyo seminari bora kuliko yote nijuayo. Kwa sababu, kazi yake ilikuwa muhimu sana hata watu wengine wasingekuwa wakimwambia, na kumpeleka nje kwa shughuli kubwa za kijamii. Unaona, alikuwa na ka—kazi, alitengwa kwa ajili ya kitu fulani. Na Yohana alijua kwamba wakati alipotoka, akihubiri, kwamba Masihi alikuwa duniani wakati huo.

153 Kwa hakika tu kama wale mamajusi walivyojua, walipotazama chini kutoka Babeli na kuona hizo nyota tatu zimepangana, hiyo ilikuwa ndiyo ishara Masihi tayari alikuwa duniani. Hiyo ndiyo sababu walikuwa wanalia, “Yuko wapi Yeye, aliyezaliwa Mfalme wa Wayahudi?” Nalo kanisa halikuwa na jibu. Hawana leo hii. Biblia ndiyo inalolo. Neno la Mungu ndilo linalo. Hiyo ni kweli.

154 Tunaona, katika yote, kwamba ilimbidi Yohana kumtangaza Masihi. Naye alikuwa... Angemjua tu Masihi huyo kwa ishara. Hivyo ndivyo alivyomjua Masihi. Hiyo ndiyo njia pekee ambayo Mungu hujitambulisha Mwenyewe; kwa ishara ya Kimaandiko. Na yeye alitazama. Alisimama pale nje, akasema... .

Wakasema, “Je! wewe ndiwe Masihi?”

155 Akasema, “La. Mimi hata sistahili kugusa viatu Vyake.” Akasema, “Lakini Yeye ni Mmoja... Yupo Mmoja aliyesimama miongoni mwenu.”

156 Loo, jamani, usifikirie kwamba nimesisimkwa! Ninajua mahali nilipo. La, bali inaleta hisi nzuri ninapoanza kufikiria juu ya hilo, unaona, “yupo Mmoja miongoni mwenu.” Na mimi ninasema hilo usiku wa leo. Yupo Mmoja miongoni mwenu, Roho Mtakatifu mkuu aliahidiwa kumwagwa katika siku ya mwisho. Ninaona ishara Yake daima, na mimi ninajua Yeye ndiye Masihi kwa sababu Yeye angali anafanya ishara ya Masihi.

157 Hapo Yeye alisimama miongoni mwao. Akasema, “Yupo Mmoja miongoni mwenu. Mimi sistahili kugusa viatu Vyake, kufungua viatu Vyake. Yeye ndiye Yule ambaye atabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto.”

¹⁵⁸ Ndipo siku moja, akitembea kutoka miongoni mwao alikuja Mtu wa kawaida, akatokea. Yohana akatazama juu, na akasema, “Tazameni, huyo hapo Mwana-kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.” Basi wakati alipofanya hivyo, aliona. Akasema, “Nilimjua Yeye kwa sababu kulikuwa na ishara iliyokuwa ikimfuata.” Basi tazama hapa, hao hapo watu wawili mashuhuri kuliko wote duniani, wamesimama uso kwa uso. Yohana . . .

¹⁵⁹ Ninamkumbuka Daktari Roy Davis, aliyeiweka wakfu katika kanisa la Baptisti ya Kimishenari, alisema, “Unajua, kilichofanyika hapo, Billy,” kasema, “kilichofanyika . . .”

¹⁶⁰ Wakati Yohana aliposema, “Nina haja kubatizwa na Wewe, na mbona Wewe waja kwangu?” Angalia unyenyekevu wa Yohana. Alisema, “Ni—nina haja kubatizwa na Wewe, mbona Wewe waja kwangu?” Huyo hapo alikuwa ni Masihi na nabii Wake, watu mashuhuri wa siku hiyo, watu mashuhuri wa Biblia, wakisimama pale, Mmoja akimtazama mwingine. Yohana katika unyenyekevu, kasema, “Nina haja kubatizwa na Wewe, mbona Wewe waja kwangu?”

¹⁶¹ Yesu akasema, “Kubali iwe hivyo, kwa kuwa inatupasa kutimiza haki yote.” Ndipo, kasema, Yohana alimkubalia.

¹⁶² Ninamkumbuka Daktari Davis. Huenda yupo ameketi. Daktari Davis, si kukutupia hili, bali mimi—mimi—mimi . . . Akasema, “Yohana, kwanza Yesu alimbatiza Yohana, kwa sababu Yohana hakuwa amebatizwa.” Ndipo basi kasema, “Ndipo Yohana akambatiza Yesu.” Hilo halikuja sahihi kwangu.

¹⁶³ Kwa hiyo siku moja wakati Roho Mtakatifu akiwa karibu, na katika ono, niliona kile kilichokuwa.

¹⁶⁴ Hapo alikuwepo Yohana na Yesu, wamesimama uso kwa uso, nabii ambaye Neno lilimjia. Nalo Neno lilikuwa limemjia nabii. Amina. Ndipo Yeye akasema, “Kubali iwe hivyo. Ilikuwa sahihi. Kubali. Lakini hivi inatupasa kutimiza haki yote.” Nabii alijua kwamba huyo alikuwa ni Mwana-kondoo, na Mwana-kondoo hana budi kuoshwa kabla ya Yeye kuwasilishwa. Amina. Kwa hiyo alifanya hivyo. Unaona hilo? Nabii, kwa kuwa ni Neno, na Hilo lilikuwa limemjia.

¹⁶⁵ [Dada fulani ananena katika lugha nyingine. Ndugu mmoja anatoa tafsiri—Mh.] Amina.

¹⁶⁶ Yohana, nabii. Neno humjia nabii Wake. Nalo Neno lilikuja hasa kwa nabii. “Inapasa,” inasema *yafaa*, ambalo linamaanisha, “inatupasa sisi kwamba tutimize haki yote.”

¹⁶⁷ Loo, jinsi ningeweza kuacha somo sasa kwa dakika moja, jinsi inavyotupasa sisi kutimiza haki yote! Saa imewadia, jambo fulani, lazima tutimize haki yote. Tunajua la kufanya. Unaona, tunapaswa kufanya hivyo, hiyo ni kweli, kuamini kwa moyo wetu wote.

168 Tazama, basi, tunakuta kwamba Yohana alijinyenyekeza katika Uwepo wa Mungu.

169 Jambo ni kwamba, watu, ndugu yangu, dada, na marafiki, ni kutambua udogo wako. Unaona? Usione jinsi ulivyo mkubwa. Tambua jinsi ulivyo mdogo. Wewe ni—wewe ni mdogo. Sote tuko hivyo. Mungu anaweza kufanya bila ya sisi, bali sisi hatuwezi bila Yeye. Unaona? Unaona? Sisi, sisi hatuwezi bila Yeye, lakini Yeye anaweza bila ya sisi.

170 Mungu anajaribu tu kumpata mtu mmoja ambaye Yeye anaweza kumshika mikononi Mwake. Daima amejaribu kufanya hivyo. Unatambua, kote katika Biblia, wakati Yeye alipompata Isaya, wakati Yeye alipompata Yeremia. Na Yeye alimpata—Yeye alimpata Samsoni, siku moja; bali Samsoni alimpatia Mungu nguvu zake, lakini akampa Delila moyo wake. Unaona, yeye. . .

171 Inakubidi kutoa yote uliyo nayo kwa Mungu; kicho chako, heshima zako, kila kitu ulicho wewe. Usiwe chochote, uone tu jinsi ulivyo mdogo, na hilo ndilo Mungu anatutaka tufanye. Na huo ni unyenyekevu wa kweli. Hivyo ndivyo hawa Maserafi walivyo katika Uwepo Wake, unaona, wakiwa na uso Wao katika kicho, umefunikwa; miguu Yao, katika unyenyekevu.

172 Sasa, la tatu, Wao waliweza kuruka. Walikuwa na mabawa mawili ambayo yaliwaingiza Wao katika matendo.

173 Mungu anamwonyesha nabii Wake hapa aina ya mtumishi ambaye Yeye amemwandaa, mwenye kicho, mnyenyekevu, na katika matendo. Huyu, unaona, huyu ni mtumishi halisi wa Mungu, hawa ambao wanamtazama Yeye. Alikuwa akimtazama Hezekia ambaye aliinuliwa juu, na akaanguka kwa kiburi. Lakini mtumishi, watumishi Wake mbele Zake, ni wenye kicho, wanyenyekevu, na katika matendo. Watumishi wake, hivyo ndivyo wanavyopaswa kuvikwa; wamevikwa kicho, unyenyekevu, na daima kwenye shughuli ya Baba. Naam, bwana. Wenye kicho, wanyenyekevu, katika matendo.

174 Kama tu vile maskini yule mwanamke, tuliyenena habari zake hivi majuzi usiku, kisimani. Sasa, yeye alikuwa ni mbegu ndogo iliyokusudiwa kimbele iliyokaa moyoni mwake, lakini, punde tu Nuru hiyo ilipoangazia juu yake hapo na yeye akaona kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi, haikumchukua muda mrefu kuingia katika matendo. Hata alisahau chungu cha maji alichokuwa nacho mkononi mwake. Hivyo ndivyo alivyoingia katika matendo upesi. Ilimbidi kuwaambia watu. Ilimbidi kumwambia mtu mwingine, kwa sababu kwamba yeye alikuwa na hakika kwamba alikuwa amempata Masihi. Huyu akaenda jijini, na upesi akaingia katika matendo, akiwaambia watu.

175 Ilikuwa ni Petro, wakati alipokuwa amevua usiku kucha, na alikuwa ameketi ukingoni asubuhi hiyo. Wakati Yesu alipoazima chombo chake, na alikuwa amekipeleka mbali kidogo kutoka ukingoni, na alikuwa akiwahubiria watu. Ndipo basi Yeye

akamwambia Simoni, “Tweka mpaka kilindini, na mkashushe kwa ajili ya kuvua samaki. Shusheni.”

¹⁷⁶ Vema, Simoni akasema, “Mimi ni mvuvi. Ni—ninajua wakati mwezi na ishara ziko sahihi. Ninajua wakati samaki wanakimbia. Ni—nilizaliwa kwenye ziwa hili hapa. Nimevuta juya usiku kucha wala sijapata hata samaki mdogo. Sijapata kitu.” Kasema, “Hakuna samaki humo ndani. Bali kwa Neno Lako,” haya basi, “Nitashusha chini wavu.” Loo, wewe huenda...

¹⁷⁷ Hatuwezi kuelewa mambo haya, wewe. Naye Mungu ni zaidi ya ufahamu. Huna budi kuamini Hilo, unaona. Mungu anajulikana si kwa maarifa, si kwa elimu. Anajulikana kwa imani, na imani pekee.

¹⁷⁸ “Kwa Neno Lako! Ninajua hakuna samaki humo. Bali Neno Lako, kama Wewe ulisema, ‘shusha chini, wapo samaki hapo,’ Wewe utatimiza, imani itawaweka hapo. Hayo ndiyo yote. Nitashusha wavu.”

¹⁷⁹ Kama watu wameketi hapa, ambao ni wagonjwa na—na wanahitaji usaidizi kutoka kwa Mungu, kama ukisema, “Nimepitia kila mstari wa maombi, ni—nimefanya kila kitu, bali, kwa Neno Lako, ninaenda kushusha wavu. Ninakuja sasa hivi, na ninaenda kupokea hilo. Ninaamini nipo katika Uwepo Wake. Na mimi...” Na utambue hilo, kwa unyenyekevu, na uaminifu na kicho. Shusha wavu. Ushikilie. Mungu alisema hivyo, na hilo hulifanya hivyo!

¹⁸⁰ Basi tunaona kwamba, punde tu yeye, akiwa ni mvua samaki na alijua kile kilichokuwa ku—kushika samaki waliojaza chombo kabisa, na yeye alikuwa ni mtu maskini, bali upesi aliingia katika matendo wakati Yesu aliposema “tangu sasa utashika watu.” Haikumchukua muda mrefu sana. Alijinyenyekeza, akaanguka chini mbele ya Kristo, kasema, “Ondoka kwangu, Bwana; mimi ni mtu mwenye dhambi.” Kasema, “Si—si—siwezi kabisa kukaa Uweponi Mwako.”

¹⁸¹ Jambo lile lile Isaya alilofanya. Alisema, “Mimi ni mtu mwenye midomo yenye dhambi, na ninaishi miongoni mwa watu wenye dhambi.” Loo, ni hali ya jinsi gani aliyokuwemo!

¹⁸² Petro alisema jambo lilo hilo, na akajinyenyekeza, akaanguka kifudufudi na kumwomba Bwana amwondokee. Akasema, “Usiogope, Petro, tangu sasa na kuendelea unaenda kuwashika watu.” Ndipo akaingia katika matendo upesi sana.

¹⁸³ Wakati mmoja, kulikuwa na mtu kipofu ambaye Yesu alimponya. Haikumchukua muda mrefu sana kuingia katika matendo; aliingia katika matendo, akieneza sifa Yake kila mahali. Mtu fulani aliinuka na kusema, “Mbona, ni nani aliyekuponya?” kuhani aliuliza. A—akasema, kamwambia ni Nani aliyemponya.

184 Kwanza waliuliza baba na mama. Ndipo mama akasema . . . Vema, sasa, waliogopa, kwa sababu kama—kama mtu yeyote angemkiri Yesu, mbona, walikuwa wanaenda kuwaondoa kwenye sinagogi. Na wao wakalirudisha juu ya maskini mwana wao. Wakasema, “Yeye ni mkubwa kutosha. Mwulizeni.”

Naye akasema, “Mmoja, Yesu wa Nazareti, aliniponya.”

185 Akasema, “Mbona, mpe Mungu sifa!” Kasema, “Sisi, sisi ndio. Hatujui chochote kuhusu huyu Yesu wa Nazareti.” Kasema, “Yeye ni mwenye dhambi. Usimpe Huyu sifa yoyote; toa yote kwa Mungu. Na sasa sisi hatujui mahali Yeye ametoka.”

186 Vema, mtu huyu kipofu alikuwa na swali zuri sana kwa ajili yao. Na yeye akasema, “Ni jambo la kigeni kwelikweli. Kwamba nyinyi nyote ndio viongozi wa kiroho leo hii, na Mtu huyu amefumbua macho yangu yaliyopofuka, na mimi nilizaliwa kipofu, na hata hivyo nyinyi hamjui mahali Yeye ametoka. Unaona, sasa hilo ni jambo la kigeni.”

187 Hivi ningeweza kusema jambo lilo hilo? Mungu yeye yule aliyeahidi kuja juu ya kanisa Lake, katika siku hii ya mwisho, nao hawana jibu. Yeye apokeaye analo jibu.

188 Kasema, “Kama Yeye ni mwenye dhambi au sivyo, siwezi kusema hilo. Ila jambo moja nijualo; ambapo nilikuwa kipofu wakati mmoja, sasa ninaweza kuona.”

189 Wakati mmoja nilikuwa mwenye dhambi; nimeokolewa kwa neema ya Mungu. Ninajua jambo fulani lilitendeka kwangu. Mimi . . . kuna jambo fulani lililotendeka. Unaweza kuliita “mtakatifu anayejibingirisha” ama unaweza kuliita chochote upendacho, lakini Hilo liliniokoa, miaka thelathini na kitu iliyopita. Na inazidi kuwa bora kila wakati, kwa hiyo ni—ninaifurahia.

Mtu fulani alisema, “Wewe umerukwa na akili.”

190 Nikasema, “Vema, basi achana na mimi. Niko vizuri zaidi hivi kuliko nilivyokuwa vile vingine, kwa hiyo nache tu nikae jinsi nilivyo. Ninajisikia vizuri zaidi hivi, na ninaendelea vyema. Ninaweza kufanya mengi zaidi.” Naam, bwana.

191 Aliingia katika matendo moja kwa moja. Naam, bwana, alieneza sifa Yake kila mahali.

192 Watu kwenye Pentekoste, punde tu walipoona kwamba Mungu alitimiza ahadi Yake! Yesu alisema, “Tazameni, ninatuma ahadi,” Maandiko, “ahadi ya Baba Yangu juu yenu. Lakini bakini,” hiyo ni *ngoja*, “ngojeni huko juu kwenye mji wa Yerusalemu hadi mtakapojazwa na Nguvu kutoka Juu.”

193 Si mstari wa kwanza wa maombi, ama wakati wa kwanza kupitia, bali kaeni tu hapo mpaka litukie, unaona. “Mpaka,” si siku moja, siku mbili, au miaka kumi, “mpaka tu litakapotukia.” Kaeni mpaka!

¹⁹⁴ Ndipo wakati walipojazwa na Roho Mtakatifu, waliingia katika matendo upesi sana; wakatoka wakaingia mtaani, na wakipiga makelele, na kucheza dansi, na kutenda kama watu walevi, na kunena katika lugha zingine, na ni kufanya yasiyofaa jinsi gani! Walikuwa katika matendo upesi sana; punde tu walipojinyenyekeza, wakaingia ndani na kufunga mlango, na kungojea juu ya Neno la Mungu.

¹⁹⁵ Loo, kile tulichoona, marafiki! Ninajua muda unaenda na sitaki kuwaweka zaidi hata kidogo. Bali, tazama! Kile ambacho tumeona, katika ninii—katika miaka michache iliyopita, kinapaswa kumweka kila mmoja wetu katika matendo. Kinapaswa kutuweka katika matendo. Nini? Kwanza, kutufanya wenye kicho, wanyenyekevu, na katika matendo. Na upendo ukiwaka mioyoni mwetu, tukijaribu kadiri tuwezavyo, kuona ulimwengu uliopotea. Na tukiona ishara ambazo Mungu. . . Hata chini, kadiri nijuavyo, hadi ya mwisho kabisa ambayo Kanisa linaenda kupokea kabla ya moto kushuka kutoka mbinguni. Nguzo ile ile ya Moto iliyoonekana kule nyuma nyikani, ile ile ambayo ilimwanguka Mtakatifu Paulo chini, ndiyo ile ile ambayo ina picha Yake iliyopigwa Yake, moja kwa moja hapa ikifanya jambo lile lile Hiyo iliyofanya kule, Masihi yule yule.

¹⁹⁶ Ukiweka uhai wa mboga ndani ya shina la tikiti maji, itazaa maboga. Ukiweka uhai wa mbalungi ndani ya m—m—mpea, utazaa balungi, kwa sababu ndio uhai ulioko ndani yake.

¹⁹⁷ Na ikiwa hiki ambacho tunakiona na kujua, maelfu kote ulimwenguni wanajua Hicho, sayansi imekishuhudia Hicho, kila mahali, picha zimepigwa. Kipo papa hapa sasa. Hiyo ni kweli, kweli kabisa. Kipo papa hapa sasa! Na kama Hicho hakitoi aina ile ile ya uhai Hicho kilitoa wakati Hicho kilipokuwa ndani ya mtu, Kristo Yesu, kama Hicho hakifanyi jambo lile lile katika Kanisa Lake, basi si sahihi. Bali ikiwa Hicho kinatoa uhai ule ule, inabidi kiwe ni Nguzo ile ile ya Moto ambayo iliongoza Israeli. Inatuelekeza kwenye Nchi ya Ahadi. “Katika nyumba ya Baba Yangu kuna makao mengi,” ahadi ambayo Yeye alitupatia, na Hiyo hutuelekeza kule. Na sisi tunaiona Hiyo ikithibitishwa kikamilifu, Neno la Mungu likidhihirishwa. Viwete wanatembea, viziwi wasikia, vipofu waona, wafu wanafufuliwa; mawazo ya moyo hayawezi kufichwa, yanatangazwa moja kwa moja, kazi zile zile ambazo Yeye alifanya. Ni kitu gani, mtu fulani? Ni Masihi! Ni Masihi, Mungu, Roho Mtakatifu, yeye Yule. Hiyo inapaswa kuweka. . .

¹⁹⁸ Kanisa la Kipentekoste, badala ya kujaribu kukosoa Hiyo, linapaswa kuwa katika matendo, kila mahali, kwa unyenyekevu na upendo, wakijaribu kumwonyesha Huyu kwa watu waliopotea na wanaokufa. Tunapaswa kumheshimu Huyu. Tunapaswa kumpenda Yeye. Tujinyenyekeze, tujifanye wenye kicho, na kuwa katika matendo kama hawa Maserafi walivyokuwa, pamoja na kicho na unyenyekevu. Akithibitishwa

wazi, aliyeahidiwa kwetu katika siku za mwisho, naye Huyu hapa! Tunamwona Yeye. Yesu alisema hivyo, kasema Hilo lingetukia. Hili hapa, kabla tu haujateketezwa. Ishara hiyo ya Kuja Kwake inathibitisha kwamba Kuja huko kumekaribia sasa. Kungeweza kuja wakati wowote. Sioni chochote cha kuzuia Unyakuo wa Kanisa hivi sasa.

¹⁹⁹ Vema, kutiwa alama, alama ya mnyama iko upande ule mwingine, kumbuka. Unaona, uasi, unaingia basi kama kanisa. Sasa ngoja, mimi, labda ningesema jambo fulani. Hiyo ndiyo njia yangu ya kuona hilo, unaona. Basi tazama.

²⁰⁰ Neno kwa neno, tayari limetimizwa. Linapaswa kutuweka katika matendo. Hiyo ni kweli kabisa. Tunapaswa kuwa tukileta kila nafsi iliyopotea, kwenye Ufalme wa Mungu, ambayo tunaweza. Kwa sababu, moja ya siku hizi unaenda kuwaleta na haitafaa kitu. Mlango utafungwa, hakutakuwako tena. Loo, huenda wakachochewa kiakili, na kusiimkwa, na kupaza sauti, na kuruka juu chini, na kudai *hili*, wajua. Lakini wakati mwanamwali aliyelala alipokuja kununua Mafuta, kamwe hakuyapata Hayo. Na hivi uliwahi kuona wakati, katika historia yote ya siku hizi za mwisho, ambapo kuliwahi kuwa na wakati ambapo Wapresbiteri, Walutheri, kila kitu kingine, kinajaribu kuja kwenye Ujumbe wa kipentekoste? Yesu alisema nini? “Wakati walipokuja kununua, ulikuwa ni wakati ambapo Bibi-arusi aliingia ndani,” bikira mwerevu aliingia ndani. Hawakupata Mafuta. Hawakuyapata Hayo. Hayo ndiyo yote. Hiyo ni kulingana na Maandiko.

²⁰¹ Nanyi mnaona ishara hizi na mambo haya mengine, kila kitu kimekaa katika utaratibu kwa ajili ya Kuja Kwake.

²⁰² Zamu ya saba, Yeye aliingia ndani. Wengine walishikwa na usingizi katika zamu ya kwanza, ya pili, ya tatu, ya nne, ya tano. Ndipo katika zamu ya saba kukaja sauti, “Tazameni, Bwana-arusi yuaja!” Wakati wa saba wa kanisa, hiyo ndiyo zamu, wakati ambao uliitazamia. Na huu ni Wakati wa Kanisa la Laodikia, mwishoni mwake. Amina. Loo, ni . . . Mbona msiamke, enyi watakatifu wa Bwana, kwa nini mnasinzia wakati mwisho unakaribia?

²⁰³ Bali, kumbukeni, kanisa katika Wakati wa Laodikia unapaswa kuwa vuguvugu. Akasema, “Kwa sababu wewe unasema kuwa ni ‘tajiri,’ na—na ‘una mali nyingi.’” Tena kasema, “Hujui kwamba uko uchi, kipofu, maskini, mwenye mashaka, nawe hujui.” Kasema, “Nitakutapika kutoka kinywani Mwangu.”

²⁰⁴ Na hapa tuko kwenye mwisho wa mambo yote, mwisho wa historia, mwisho wa ustaarabu. Unaweza kuona. Tazama nje mtaani.

²⁰⁵ Nilikuwa nikizungumza na dereva wa tekisi, alikuwa akinileta huku. Akasema, “Vema, njia ya pekee niwezayo kujua,

nikiona mtu akitenda hapa kama mwenye akili timamu, ninajua yeye ni mgeni.” Unaona? Sasa, huyo ni mmoja wa madereva wenu wa tekisi aliyesema hilo. Kasema wangeninii. . . njia.

²⁰⁶ Si hapa tu, bali ni kila mahali. Mwisho wa kila kitu; jinsi walivyo katili, watu, na kila namna ya mambo maovu, na kile wao wanafanya. Ulimwengu umepotoka. Tazama nje mitaani. Utazame tu, loo, jamani, kila mahali! Sio tu katika Marekani; kila mahali, mbona, ni—ni Sodoma mamboleo.

²⁰⁷ Hakuna kitu cha kubakishwa, ila kuteketezwa. Na, hayo ndiyo yote, utafagiliwa mbali. Mungu atafanya hivyo. Sheria zake zinahitaji hivyo. Haina budi kufanywa hivyo. Wakati ubua wa mahindi umemaliza wakati wake, hauna budi kuangamizwa. Wakati ua likimaliza wakati wake halina budi kufa. Nao ustaarabu umemaliza wakati wake. Wakati wa kanisa umemaliza wakati wake. Madhehebu yamemaliza wakati wake.

²⁰⁸ Huu ni wakati wa kuunganika. Kuna Muungano wa Taifa, kanisa lililoungana, na juhudi zilizoungana. Ni ishara ya nini? Kristo na Bibi-arusi Wake wanaungana. Hilo ndilo lililo. Yote ni vivuli na mifano. Kila kitu kinataka kushirikishwa, kwa hiyo ni ishara. Kristo anajiandaa kuungana na Bibi-arusi Wake, Karamu ya Arusi inafanyika angani, kwa hiyo inapaswa kulingiza kanisa katika matendo wakati tukiona ishara Zake hapa zimewadia. Loo, jamani! Mambo haya yote ni ishara kwetu, kila mahali. Loo, tunapaswa kuwa katika matendo!

²⁰⁹ Sisi, kama nabii wa kale, Isaya, tunaona kile ambacho watu waliojiinua hufikia. Tunaona kile, madhehebu haya yanayoinuka na kusema, “Vema, kwa sababu wewe si mmoja wetu, wewe hata huko ndani yake,” tunaona kile kinachowafanyikia. Wanapoteza nini? Kama tu vile wamepigwa na ukoma wa dhambi, na kutokuamini, wao—wao wanapoteza msimamo wao kwenye Neno la Mungu. Baadhi ya watu hawa wanajaribu, wanabadilisha, wanapoteza msimamo wao juu ya Neno, na kubadilisha Hilo na kanuni za imani. Wanajipatia kitu gani? Mchafuko wa ukoma. Hiyo ni kweli.

²¹⁰ Kama vile Uzia wa kale, akijaribu kuchukua mahali pa ofisi iliyotiwa mafuta, na hana chochote ila shahada ya udaktari, au kitu fulani. Mungu haangalii shahada ya udaktari; Yeye anaangalia mioyo minyenyekevu, mtu fulani ambaye atamwamini Yeye. Lakini tumechukua wanaume na kuwaelimisha kuwa maaskofu na kila kitu kingine, makadinali na chochote zaidi, tukawaelimisha vya kutosha kushikilia ofisi ya Kiungu pamoja na elimu ya kimwili. Tunahitaji ubatizo wa Roho Mtakatifu, kuchukua ofisi hiyo. Roho Mtakatifu ndiye Mwalimu wetu. Yeye ndiye Ambaye hujifanya Mwenyewe kujulikana miongoni mwetu, ishara ya wakati, siku za mwisho. Lakini sisi, kama Hezekia, tumeinuliwa, wanafikiria tu kwamba wanaweza kuchukua mahali pao.

²¹¹ Angalia kile matokeo ya ono yalimfanyia nabii. Sasa, yeye alikuwa nabii. Alikuwa chombo kwa ajili ya Neno la Bwana kujia. Alichaguliwa, akazaliwa nabii. Hatimaye akatoa maisha yake, akakatwa vipande vipande kwa msumeno. Bali tunaona ya kwamba nabii huyu mashuhuri, wakati alipoona ono hili kutoka Mbinguni, na kuona utaratibu, jinsi Mungu alivyokuwa anatarisha watu Wake, mbona, ilimsababisha nabii kukiri kwamba yeye alikuwa ni mwenye dhambi.

²¹² Na sisi tunataka kuwa wakubwa sana, na kuvaa namna fulani ya ukosi mkubwa uliopinduliwa, namna fulani ya nguo, mwajua, zinazotufanya kuonekana watakatifu sana na wenye kicho. Hakuna utakatifu kwetu sisi. Hatuwezi kuwa watakatifu; utakatifu ni wa Mungu. Unaona? Hakika. Si kanisa takatifu, si mlima mtakatifu; ni Mungu mtakatifu. Hiyo ni kweli. Si watu watakatifu; Mungu mtakatifu! Ni Mungu ndani ya watu. Petro alitaja Mlima wa Kugeuka Sura, “mlima mtakatifu,” ilimaanisha kuwa Mungu mtakatifu alikuwa juu ya mlima. Iangalie sasa, unaona. Lakini ilikuwa ni Mungu mtakatifu huko, Uwepo wa Mungu, uliufanya kuwa mtakatifu.

²¹³ Ni Uwepo wa Mungu katikati yetu sasa unaoleta utakatifu, si utakatifu wangu, si wako, bali utakatifu Wake. Uwepo Wake ndio ambao huleta utakatifu. Tunapaswa kujinyenyekeza, tujifunike katika kicho, unyenyekevu, na kusema, “Bwana Yesu, nipokee katika Ufalme Wako.” Utakatifu Wake, si wetu. Roho Mtakatifu!

²¹⁴ Nabii aliungama, ilimsababisha kusema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu.” Nabii! Mungu, tunahitaji ono jingine kama hilo! Wakati alipoona huko juu, ninii . . . aliona Nguvu hii ya Mungu itakasayo.

²¹⁵ Sasa angalia jinsi Mungu alivyofanya. Alimtuma mmoja wa Maserafi na akachukua koleo, akachukua kaa la moto kutoka kwenye madhabahu na kuliweka mikononi Mwake, akaja akaweka kichwa cha Isaya nyuma na kugusa midomo yake, kasema, “Uovu wako umeondolewa.”

²¹⁶ Ndipo Isaya akajifunza somo jingine. Huenda nikaingiza hili ndani. Huenda halifai sana, lakini ninaamini linafaa. Hivi ulitambua, Mungu huwatakasaa manabii Wake kwa Moto, si kwa theolojia au kitabu cha namna fulani. Unaona? Yeye huwatakasaa watu Wake kwa Moto, Roho Mtakatifu na Moto; si kwa taarifa ya kanuni za imani, ama vitabu au kitu fulani ambacho inakubidi kujifunza, lundo la maombi, na kadhalika. Yeye huwatakasaa kwa Moto kutoka kwenye madhabahu. Hivyo ndivyo Yeye humweka katika utaratibu. Naam. Naam, bwana. Hivyo ndivyo Yeye alivyowatakasaa manabii Wake hapo mwanzo, wakati watu mia moja na ishirini walikuwa katika chumba cha juu, Roho Mtakatifu alishuka, na ndimi za Moto zikawakalia juu yao. Walitakaswa na tayari kwa utumishi. Hivyo ndivyo

Mungu hutakasa. Si kwa masomo, kupata Shahada ya Kwanza ya Sanaa, ama DD., Ph.D.; bali kupata Moto Mtakatifu kutoka Mbinguni, ambao huondoa uongo kutoka midomoni mwako, na kuondoa ubinadamu kutoka kwako, huchoma na kuondolea mbali upuuzi huo, takataka hiyo ya—ya ulimwengu, na kuweka Uwepo Wake mle ndani na kuishi kupitia mtu huyo. Moto Mtakatifu ndio ambao Mungu hutakasa Kanisa Lake kwao. Isaya alijifunza hilo. Tunapaswa kujifunza hilo, kwamba Mungu hatakasi kwa maarifa. Yeye hutakasa kwa Moto.

217 Unaona jinsi alivyo, nabii aliyeandaliwa. Sasa Yeye alitakasa midomo yake, akaondolea mbali uovu wake. Ndipo baada ya kufanya hivyo, akakiri, akajinyenyekeza, akasema, “Mimi ni mtu mwenye midomo michafu,” wakati alipoona Uwepo wa Mungu.

218 Je! mnanifuata? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Ni nini sisi, ni nini tunachojua sisi sasa hivi? Tuko katika Uwepo wa Mungu. Hiyo ni kweli. Hivi sasa tumeketi. Je! nyinyi... Hatuwezi kufahamu hilo, bali tuko katika Uwepo wa Mungu sasa, tunamwona Mungu. Je! mnaamini Yeye yupo hapa? [“Amina.”] Hakika, Yeye yupo hapa. Sisi...[Sehemu tupu kwenye kanda.]

219 Mimi ni ndugu yenu. Lakini Yeye alisema, “Kazi nizifanyazo, Yeye ataninii...nanyi pia mtazifanya.” Je! hilo ndilo Yeye alilosema? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Vema. Kama Yeye yupo hapa, Roho Wake yupo hapa. Hilo ndilo humfanya Yeye. Basi ikiwa sisi tunaweza kujisalimisha na kuondolea mbali mawazo yetu wenyewe. Kama tu vile *hii* haina mawazo yoyote, basi sauti nyingine inaweza kunena kuipitia. Hiyo ndiyo njia. Kama tunaweza kujifanya tupu sisi wenyewe. Hiyo hapo ndiyo siri, jiondoe mwenyewe! Halafu Mungu anapata... Ondolea mbali mawazo yako mwenyewe. Ondolea mbali njia zako mwenyewe, na ndipo umrusu Mungu kutembea. Kama Yeye ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo na hata milele, mnaamini hilo? [“Amina.”] Wewe mwamini Yeye sasa hivi na uone kama ni hivyo.

220 Nimekuwa nikimtakama jamaa huyu mdogo aliyeketi hapa, papa hapa mbele zangu. Huna kadi ya maombi. Wewe, ikiwa Mungu ataniambia kilichokufanya uketi hapo, unaamini? Ni shida ya kiroho, umefungwa kabisa na hujui jambo la kufanya. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema, yote yamekwisha. Lichukue Neno, kile ambacho nimesema, na yote yamekwisha.

Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

221 Mama huyo mweusi anayeketi moja kwa moja hapo nyuma, akimtakama; anao ugonjwa wa moyo. Je! unaamini kwamba Mungu atakufanya mzima? Hakika. Unaamini? [Dada huyo anasema, “Amina.”—Mh.] Vema, unaweza kupata uponyaji wako.

Je! unaamini Yeye ni yule yule jana na... .

222 Mwanamume huyo, huyo mzungu aliyeinua mkono wake, je! unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu, mtumishi Wake? Sikujui. Wewe ni mgeni kwangu. Una kadi ya maombi au chochote? Wewe ni mwanaume tu aliyeketi hapa. Vema, bwana, una kivimbe katika koo lako. Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli? Je! unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Unaniamini mimi kwa moyo wako wote? Una jingine, una mzigo moyoni mwako. Ni kuhusu msichana mdogo, mjukuu wako. Ana mkono mbaya. Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli? Kuna mwuungano mzuri. Hebu kidogo. Wewe hutoki hapa. Umetoka Connecticut. Nalo jina lako ni Wilson. Jina lako la kwanza ni Art. Art Wilson. Hiyo ni kweli kabisa. Je! hiyo ni kweli?

Je! mnaamini? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kweli!

223 Yupo mama anayeketi moja kwa moja hapa nyuma, mama mweusi, anaonekana kama amevaa kitu kama koti la manjano, naam, kijani kibichi cha divai. Anaomba. Una kadi ya maombi? [Dada huyo anasema, “Sihitaji yoyote!”—Mh.] Huna kadi ya maombi? Huna. Unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Mimi ni mgeni kabisa. Sisi ni jamii mbili za watu. Wewe, lakini unaomba. Huyo ni wewe. Naam. Je! unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yako? Una kivimbe. Hiyo ni kweli. Unalo jambo fulani moyoni mwako, pia. Unaomba. Ni rafiki, ana shida ya figo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Sasa unaweza kupata haja yako.

224 Ninaisai imani yako! Ni kitu gani? Wakati nabii alipoona kwamba alikuwa katika Uwepo wa Mungu, alijinyenyekeza. Tazama, kwanza alijinyenyekeza, ndipo Moto ukamtakasa. Na baada ya Moto kumtakasa, basi ilikuwa ni Isaya aliyetakaswa. Wakati aliposikia Sauti ya Mungu, kasema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili Yangu?” aliingia katika matendo, “Mimi hapa, nitume mimi.” Loo, jamani!

Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,
Likimfanya kuwa safi kabisa,
Wakati Sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?”
Ndipo akajibu, “Bwana, mimi hapa, nitume mimi.”

225 Amina. Huo ulikuwa ndio wito wa Isaya aliyetakaswa, baada ya Roho Mtakatifu kumtakasa. Hakuhitaji ujuzi wowote wa kiseminari, hakuhitaji ujuzi wowote wa kitabuni. Alikuwa ametakaswa na Moto wa Mungu, na kuitwa kuingia katika matendo. Kilikuwa ni kitu gani? Wakati alipomwona Mungu katika matendo, aliingia katika matendo.

226 Tunamwona Mungu katika matendo. Ni wakati kwa ajili ya kanisa kuingia katika matendo na kuwa mifano ya kile Mungu alichu. Je! mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

Ni wangapi wanataka kuungama makosa yenu yote na kila kitu sasa, na kusema, “Mungu, nitakase”?

Mponye mvulana huyo.

Wakati kaa la Moto lilikuwa limemgusa nabii!

²²⁷ Hebu tusimame kwa miguu yetu. Nitakomea papa hapa, muda unaenda sana. Amini kwa moyo wako wote sasa.

²²⁸ Ninawatakeni muinamishe vichwa vyenu. Kumbukeni, baada ya yeye kumwona Mungu! Hiyo hapo tena! Amina. Sasa chochote chaweza kutokea. Chochote chaweza kutokea.

Wakati kaa la Moto lilipokuwa limemgusa nabii,

Likimfanya kuwa safi kabisa,

Wakati Sauti ya Mungu iliposema, “Ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu?”

Ndipo akajibu, “Mimi hapa, nitume mimi.”

Nena, Bwana wangu, (inueni mikono yenu sasa) loo, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitakuwa mwepesi kukujibu Wewe;

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

Loo, mamilioni sasa wanakufa katika dhambi na aibu, (tazama kwenye mitaa yenu)

Loo, kisikie kilio chao chenye huzuni na uchungu;

Loo, hima, ndugu, hima kwa ajili ya wokovu wao;

Upesi jibu, “Bwana, mimi hapa.”

Nena, Bwana wangu, (maanisha kabisa sasa) nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitakuwa mwepesi kukujibu Wewe;

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, “Bwana, nitume mimi.”

²²⁹ Hebu tuweke mikono yetu juu ya moyo wetu, huku tukivumisha. Fanya ungamo lako, useme, “Bwana, mimi ni mwanaume mwenye midomo michafu. Mimi ni mwanamke mwenye midomo michafu.” Hebu tuwe na maungamo halisi, tutakuwa na uamsho kwelikweli. Kwanza utakaswe. Angalia, ilibidi nabii atakaswe kwanza. Moto ulingusa, ndipo akaingia katika matendo. “Bwana, nipe juhudi moyoni mwangu. Weka kitu ndani yangu ambacho sina, Bwana. Weka upendo Wako na Moto ndani yangu, ndipo unitume.” Sasa fanya maungamo yako, mwamini Mungu kwa moyo wako wote.

Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
 Loo, nena, nami nitakujibu Wewe upesi;
 Nena, Bwana wangu, nena, Bwana wangu,
 Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

[Ndugu Branham anaanza kuvumisha—Mh.]

Likimfanya safi kabisa,

Wakati Sauti ya Mungu iliposema, "Ni nani
 atakayekwenda kwa ajili yetu?"

Ndipo akajibu, "Bwana, hapa, nitume mimi."

²³⁰ "Nena." Sasa mwache Mungu anene na moyo wako sasa; kwa unyenyekevu kabisa, kwa utamu, kwa kicho katika Uwepo Wake. Kila mwenye dhambi, kila mtakatifu, hii ni kwa ajili yetu sote. Ni kwa ajili yangu. Ni kwa ajili ya wote. Huu hapa Uwepo Wake, Yeye yupo hapa kile Yeye alichosema Yeye angefanya. Ishara ambayo Yeye alisema tungepata, Yeye huyu hapa. Huku muziki ukipigwa kwa utamu, hebu tukiri tu makosa yetu. "Mimi si kitu bure, hata hivyo, Bwana. Nena na moyo wangu. Nitakase kwanza, Bwana. Mtume Roho Mtakatifu na unitakase. Ninajua nipo katika Uwepo Wako. Ninakuona Wewe kama Isaya alivyokuona Wewe, ukitembea. Mahali pamejaa, si moshi sasa, pamejaa Nuru, pamejaa Utukufu."

²³¹ Ee Bwana Mungu, Muumba wa mbingu na nchi, wakati hili likiwa niani mwetu, tunaona kile kinachofanyika kwa watu walioinuliwa juu. Wote walikuwa ni mifano kwetu. Tunaona kile unyenyekevu na maombi, kwa waliokolewa, kinachomaanisha.

²³² Ninaomba, Baba wa Mbinguni, sasa hivi tu kwa ajili ya kusanyiko hili na kwa ajili yangu mwenyewe. Bwana, ondoa kwangu chochote ambacho si kama Wewe. Ni—ni—ni—ninakutaka Wewe uishi ndani yangu, Bwana. Ninataka Roho Wako pamoja na—pamoja na utangulizi. Ninakutaka Wewe uishi kikamilifu sana ndani yangu, hata si mimi mwenyewe tena, kwamba ni—nitembee tu na kuzungumza na kuishi ndani Yako. Tujalie, Bwana. Mimi hapa. Nitakase, Bwana. Litakase kanisa hili. Tutakase sote, pamoja. Ondoa ugonjwa, ondoa dhambi, ondoa kutokuamini, ondoa shaka, ondolea yote mbali. Naomba Roho Mtakatifu aje sasa akiwa na kaa la Moto kutoka Madhabahuni, cheche mpya ya pentekoste, na kutakasa kila moyo hapa ndani. Tutwae, Bwana. Sisi ni Wako. Tunakuamini Wewe. Tujalie, Baba.

Nena, Bwana wangu,

Nena, nami nitajibu, "Bwana, nitume mimi."

²³³ Wote wanaotaka, na watafanya, na mmeweka wakfu maisha yenu kwa Kristo, upya, sasa hivi, na unataka kujiweka wakfu katika Uwepo Wake!

²³⁴ Kama ningeanza kuita kile ambacho nimeona, ninge... ingechukua kila mtu humu ndani, ninaamini, sasa hivi. Ninawajua. Mnajua nisingesimama hapa na kusema hilo kama

mtumishi wa Kristo bila ya Hilo kuwa tu kila mahali. Mko katika hali sasa hivi kuanza pentekoste mpya. Hiyo hakika ni kweli, marafiki.

²³⁵ Jinyenyekezeni tu. Funika uso wako, funika miguu yako, mkaribie tu Yeye. Inama chini na ufanye maungamo yako, na uamini. Je! unataka kufanya hilo? Kama mnataka, inueni tu mikono yenu, wakati tukiimba “*Nena, Bwana Wangu.*”

Nena, Bwana wangu, (ombeni sasa) nena,
Bwana wangu,

Nena, nami nitakuwa mwepesi kukujibu
Wewe;

Loo, nena, Bwana wangu, nena, Bwana
wangu.



USHAWISHI SWA63-1114

(Influence)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Alhamisi jioni, tarehe 14, Novemba, 1963, katika Marc Ballroom kule New York, New York, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org